SportPesa
TZS. 642,668,240
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**EWURA** kuanza msako wa vituo, maduka bubu kuuzia mafuta nchini

UKURASA 3


Nipashe TESA
Jumanne Novemba 2, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 12
Utaalamu ETV unavyoongeza matumaini tiba kichwa kikubwa

Ukurasa 13
Pongezi ujio wa vitabu, kazi ni kujenga hamasa kusoma

Ukurasa 14
Mbunge alipoonyesha uliko ufunguo wa kufaulu sayansi

ELIMU
NA MWANDISHI WETU, DODOMA

'Laiti' serikali ingetumia utafiti, ripoti isingepoteza trilioni 1.2/- kila mwaka

KAMA serikali ingechunguza na kufahamu mbinu, na kama ingetumia ripoti za utafiti na taarifa za wataalamu za kitafiti na kutumia mbinu na mikakati ya kuziba mianya ya ukwepaji kodi unaofanywa na kampuni za kimataifa kwenye sekta ya uziduaji hasa madini, Tanzania isingebaki hivi ilivyo leo.

Ni kilio cha vyama shiriki vya shirikisho la asasi zinazotoa huduma kwa umma duniani (PSI) pamoja na asasi za kiraia (AZAKI) nchini zikiomba serikali kutumia ripoti hizo kukomesha ukwepaji kodi kwenye sekta ya uziduaji (kuchimba madini, mafuta na gesi), hasa eneo la madini unaoliumiza taifa.

Wakizungumza jijini Dodoma kwenye jukwaa lililowakutanisha wadau hao wanasema wakati umefika, serikali ihakikishe Watanzania wanapata elimu ya kuzijua rasilimali hizo, kuiona mikataba ya uwekezaji wake, wanapata taarifa za mienendo ya kampuni hizo zinazochimba madini na zaidi kuhakikisha kuna uwazi kwenye uwekezaji kwenye uziduaji.

Wanaasasi za kiraia na wataalamu wanasema laiti kampuni za madini zingelipa kodi stahiki na kwa wakati, serikali ingepata fedha nyingi za kugharamia huduma muhimu za jamii kama vile elimu, afya na miundombinu ya barabara mijini na vijijini.

Kadhalika mapato hayo yangeinua sekta nyingine kama kilimo na kuzalisha ajira nyingi, wanasema washiriki wa mkutano huo unaoandaliwa na Shirika la Friedrich Ebert Stftung (FES) la Ujerumani kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama Vinavyotoa Huduma kwa Umma Duniani (PSI).

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa FES Elisabeth Bolrich, anasema idadi ya watu inaongezeka, ni vyema sekta ya uziduaji itumike vyema kupata fedha za kusaidia huduma za jamii mfano elimu, afya na miundombinu kuwafikia raia wanaoongezeka.

Meneja uchambuzi wa bajeti na sera kutoka Shirika lisilo la kiserikali la Policy Forum, Nicholas Lekule, anamuunga mkono akisema wakati umefika serikali kuhakikisha kila mtu na kila kampuni inayofanya shughuli zake nchini inalipa kodi stahiki.

Anasema mapato kutoka sekta ya madini ni muhimu kwa ajili ya huduma za jamii na miradi mikubwa kama miundombinu ya barabara na mradi wa kufua umeme wa bwawa la Mwalimu Nyerere.

"Ukiangalia bajeti ya nchi miradi mikubwa ya maendeleo inategemea wafadhili wa nje na mikopo. Lakini kama kila kampuni ya madini ingelipa kodi stahiki, miradi mingi ya maendeleo na huduma za jamii kama afya, elimu na barabara, ingejengwa kwa kiwango cha juu na mapato yatokanayo na kodi." Anasema Lekule.

Utafiti unaofanywa na Shirika la Action Tanzania mwaka 2020/21 Tanzania inapoteza Dola milioni 531 takribani Shilingi trilioni 1.2 kila mwaka kutokana na misamaha ya kodi kwenye sekta ya uziduaji, anasema Dk. Balozi Morwa.

Dokta Morwa, Mshauri wa Kodi wa shirika hilo, anasema lengo la kampuni yoyote ni kupata aida. Kwa hiyo kampuni zina mbinu mpya, ujuzi, teknolojia na utalaam sana na wakati mwingine kushinda wataalam wazawa.

Waziri wa Madini, Doto Biteko. PICHA: MTANDAO

Anasema serikali isipokuwa makini ni lazima ipate hasara kutokana na utalaam wao wa kukwepa kodi.

"Wakati ufike mikataba yao iwekwe wazi, ipitiwe upya na ifuatiliwe kwa kina nje na ndani ya nchi ili kuziba mianya yote ya uwepaji kodi."

Anaungwa mkono na mbunge Cecilia Pareso (viti maalum Arusha), anasema kutokana na utafiti na taarifa za watafiti, nchi inapoteza kiasi kikubwa mno cha fedha kutokana na makampuni kukwepa kodi na misamaha ya kodi.

"Wito wangu kwa serikali ni utashi wa kisiasa, watumie hizi tafiti za wataalam vizuri kuziba mianya ya ukwepaji kodi unaofanywa na kampuni mbalimbali," anashauri.

Pareso ambaye ni makamu mwenyekiti wa mtandao wa wabunge wa Afrika wapambanaji wa rushwa anasema Tanzania ina sera na sheria za madini nzuri, lakini tatizo ni kwenye utekelezaji na kuishauri serikali itekeleze sera na sheria zilizopo.

Mbunge Constantine Kanyasu wa Geita Mjini, anatoa wito kwa Watanzania kuwa makini katika kusaini mikataba ya madini na kuwataka waungane kufichua wakwepa kodi na rushwa kwa ujumla.

"Kila mtu, Bunge na taasisi mbalimbali zina kazi ya kufanya kutimiza wajibu, tukifanya hivyo tutakuwa tumesaidia serikali kukusanya mapato kwa wingi," anasema.

Mratibu wa Haki Kodi (Tax Justice Project), Daniel Oberko, wa PSI anasema kuwa utekelezaji wa sera na sheria ni lazima ili kukabiliana na ukwepaji kodi kunahitajika utashi wa kisiasa.

Anakumbusha kuwa hilo linawezekana pale kutakapokuwa na mifumo thabiti ya serikali inayofanya kazi kwa uwazi na ushirikiano wa karibu na wadau wote.

"Serikali lazima iamue kuwa inakwenda kutumia mapato kujenga nchi na miradi ya maendeleo ikiwamo huduma za jamii kama elimu, afya na barabara na kuendeleza sekta nyingine kama kilimo na kutengeneza ajira.

Amezitaka AZAKI, vyama shiriki vya PSI na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) na vyama vya wafanyakazi kama TUGHE,

INAENDELEA UK.12


Nipashe
Jumanne Novemba 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580752
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11



# Video maburungutu fedha zatua kortini

**NI** ushahidi dhidi ya Sabaya madai wakichukua fedha benki zikiwa kwenye boksi... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mjumbe Maalum wa Waziri Mkuu wa Uingereza katika masuala ya biashara kati ya Tanzania na Uingereza, Lord Walney, jijini Glasgow, nchini Scotland. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 4

## AZAKI ZATOA NENO KUFUKULIWA KABURI LA MWILI MWENYE UALBINO

WANAHARAKATI na watetezi wa haki za binadamu wameibuka na kulaani kitendo cha kufukuliwa kwa kaburi la mtu mwenye ualbino, Heri Kijangwa, na kunyofoa mguu kisha kutoweka nao.

UKURASA WA 4

## NEMC YAKIRI UJENZI MABONDENI TATIZO SUGU

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema ujenzi holela kwenye mabonde na mito bado ni tatizo kubwa linalosumbua hasa kwenye mkoa...



# Kibano shahidi kesi Mbowe saini, maelezo kutofautiana

UKURASA 2

## Chanjo corona dozi 500,000 kutoka China zawasili Dar

UKURASA 3

MICHEZO YANGA, RUVU ZAIDI NI YA 'PIRA SAMBUSA' LEO UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa jarida la UNICEF likiwa na ujumbe wa 'Maliza Ukatili na Udhalilishaji Dhidi ya Wanawake na Watoto Zanzibar' na Mwakilishi wa UNICEF Zanzibar, Laxmi Bhawani, wakati wa mazungumzo yao yaliofanyika ukumbi wa Ikulu jijini Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# Video maburungutu fedha kesi Sabaya zatua kortini

**Na Allan Isack, ARUSHA**

VIDEO sita zilizokuwa kwenye 'flash' zimepokewa mahakamani kama kielelezo cha ushahidi kwenye kesi ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, huku watu wawili wakionekana kuingia ndani ya benki wakitoa na kuchukua maburungutu ya fedha ambazo ziliwekwa kwenye boksi.

Flash hiyo, iliwasilishwa mahakamani na shahidi wa nane wa Jamhuri, Johnson Kisaka (35), kama kielelezo cha ushahidi.

Sabaya na wenzake walipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, wakikabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi. Washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya.

Video hiyo ilionyesha watu hao wawili wakiingia katika benki hiyo, Januari 22 majira ya 10:10 na kutoka saa 11:03 na baada ya kutoka na hela hizo waliingia nazo kwenye gari lenye rangi ya bluu.

Wakati huo, ofisa wa benki hiyo alifika katika eneo la mapokezi "Kaunta" akiwa ameshika boksi mkononi na kuanza kuzipangilia fedha ndani ya boksi hilo na baada ya kukamilisha mchakato wa kuhakiki fedha hizo, aliziweka juu ya kiti cha kuzunguka na kupeleka kuwakabidhi wahusika.

Watu hao walitoka kwenye benki hiyo wakiwa wamebeba boksi hilo kwa pamoja. Kadhalika watu hao, mmoja akiwa mtu wa makamo, alivaa koti kubwa kama mtu anayefanya kazi gereji huku mwenzake akiwa ni kijana.

Wakati mchakato mzima ukiendelea wa kusubiri fedha kutolewa benki, kijana huyo alikuwa akiimarisha ulinzi huku akizunguka benki na kumfuata nyuma mzee kila sehemu alipokuwa anakwenda na baada ya kuchukua maburungutu ya fedha hizo, waliondoka pamoja.

Pia video hiyo ilionyesha kijana huyo akiwa amevaa fulana ya mistari, kofia nyeusi na suruali nyeusi.

Shahidi huyo, alidai video za CCTV kwenye Benki ya CRDB zilitolewa tawi la kwa Morombo, jijini Arusha.

Alidai baada ya kutoa ushahidi huo, alimkabidhi Ramadhani Juma ambaye ni Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

**PINGAMIZI LATUPWA**

Awali, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, inayosikiliza kesi hiyo chini ya Hakimu Mkazi, Pastricia Kisinda, ilitupilia mbali pingamizi la mawakili wa utetezi, juu ya kupokewa mahakamani kwa flash yenye video sita.

Akitoa uamuzi mdogo kuhusu pingamizi hilo, Hakimu Kisinda alisema baada ya mahakama kupitia kifungu cha 64A cha Sheria ya Ushahidi Namba 6 ya mwaka 2019 na kifungu cha 18(1), (2) cha Sheria Kielektroniki namba 13 ya mwaka 2015, vielelezo hivyo vimekidhi vigezo vya kupokewa.

Oktoba 28, mwaka huu, mawakili wa utetezi walipinga kupokewa kwa flash ambayo ndani imewekwa video sita kama kielelezo cha ushahidi kwa madai kuwa hazikuonyeshwa kabla ya kukubaliwa kupokewa.

Pingamizi hilo liliwasilishwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, kabla ya kuwasilishwa na shahidi wa nane wa Jamhuri, Jonson Kisaka (35), ambaye ni ofisa wa maabara ya uchunguzi wa kielektroniki kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Nyaraka nyingine zilizopingwa kupokewa kama vielelezo vya ushahidi na mawakili hao ni fomu namba 28 na 29 pamoja.

Katika pingamizi hilo, Mahuna alidai kuwa vielelezo hivyo ikiwamo flash, shahidi huyo alifungua ripoti mwanzoni bila kucheza video sita zilizopo ndani yake. Mahuna alidai kwamba sheria inaelekeza wanapotoa vielelezo vinatakiwa kupitiwa au kufungua video hizo ili kutambua ni kitu gani kimewekwa.

Pia alidai kwamba sheria imeelekeza na inataka kupatiwa kielelezo hicho kwa mapana yake ili kutambua ni kitu gani kimo ndani ya kifaa hicho.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, alidai utaratibu wa kisheria wa kuwasilisha vielelezo hivyo umezingatiwa kwa kuwa shahidi ameonyesha vitu ambavyo amevizungumzia wakati akitoa ushahidi wake wa msingi.

Alidai kuwa Sheria ya Kielektroniki kifungu cha 15 hakijaeleza kuwa kielelezo kinatakiwa kusomwa ndipo kipokewe mahakamani.

Naye Othmed Mtenga, Wakili wa Serikali Mwandamizi, aliiomba mahakama kupokea flash hiyo na nyaraka nyingine kwa kuwa wamefuata utaratibu wa kisheria.

Alidai kuwa hoja hizo haizuii flash na nyaraka kupokewa kwa kuwa kinachoangaliwa ni kama shahidi anautambua ushahidi anaouzungumzia na kama amehusika kuuandaa. Pia alidai kisheria shahidi anatakiwa kuelezea kielelezo hicho kabla ya kukitoa mahakamani.

"Tunaiomba mahakama kupokea kielelezo hiki kwa kuwa shahidi ameeleza kwamba anakifahamu. Pia hoja ya kusema kielelezo kionyeshwe nini kilichomo ndani ni sawa na kukifungua kabla ya kupokewa kwanza kwa kuwa kiutaratibu unatakiwa kupokelewa ndipo kisomwe mahakamani," alidai.

# Kibano shahidi kesi Mbowe saini, maelezo kutofautiana

**Na Elizabeth Zaya**

SHAHIDI wa nne katika kesi ya tuhuma za ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, na wenzake watatu, Anitha Valerian (45), jana alipata wakati mgumu baada ya kubanwa na mawakili wa utetezi kutokana na madai kuwa saini zake na maelezo aliyotoa polisi na mahakamani vinatofautiana.

Valerian (45) mkazi wa Ruwa, Moshi mkoani Kilimanjaro, alihojiwa kwa takribani saa tano na mawakili hao wakiongozwa na Peter Kibatala katika kesi hiyo inayosikilizwa na Jaji Joachim Tiganga katika Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi.

Shahidi huyo, baada ya kumaliza kuhojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Esther Martin, kwa takriban dakika 45, ndipo alipoanza kuulizwa maswali na mawakili wa utetezi.

Wakili wa utetezi aliyeanza kumhoji ni Jeremiah Mtobesya na baada ya maswali kadhaa, aliomba apatiwe nakala ya maelezo ya ushahidi aliyotoa polisi ambayo iliwasilishwa mahakamani. Pia alitaka mahakama hiyo iruhusu shahidi athibitishe saini aliyotia katika maelezo yake.

Hapo ndipo yalipoibuka mabishano ya kisheria, hivyo kumfanya Jaji Tiganga kuamuru kwenda mapumziko kwa dakika 10 ili kutoa muda wa majadiliano kwa ajili ya jambo hilo.

Saa 6:15 kesi iliendelea tena na Jaji kuamuru upande wa utetezi upatiwe nakala kwa ajili ya matumizi mahakamani hapo na baadaye kurejesha. Baada ya kupewa, Mtobesya aliendelea na kuuliza maswali.

Kabla ya kuendelea na maswali, Mtobesya alimpatia shahidi nakala hiyo ili aisome kuthibitisha maelezo hayo aliyotoa Agosti 5, mwaka jana, katika kituo cha polisi cha Moshi pamoja na saini kama ni vyake. Shahidi alikubali kwamba vyote ni vyake.

Baada ya shahidi huyo kusoma na kuthibitisha kwamba ni vyake, Wakili Mtobesya alionyesha kutokuridhika kwa madai kwamba yale aliyoyaeleza wakati akihojiwa na Wakili Martin, baadhi hayakuandikwa kwenye nyaraka iliyowasilishwa mahakamani hapo kwa ajili ya kutumika kama ushahidi. Alipomhoji, shahidi huyo alikiri kwamba ni kweli baadhi ya maelezo hayakuandikwa katika nyaraka hiyo.

Pia Mtobesya alidai kwamba baadhi ya nyaraka zilizowasilishwa mahakamani ambazo shahidi alikiri kuwa alitia saini, zilikuwa zinapishana saini na alipomhoji sababu za saini hizo kupishana, alidai kuwa zingine alitia saini akiwa amesimama na zingine akiwa amekaa.

Baada ya Mtobesya, Wakili John Mallya alisimama na kumhoji kutaka kufahamu endapo shahidi huyo alikuwa anafahamu majina ya askari polisi waliowakamata vijana hao. Shahidi huyo alidai hakufahamu majina yao ingawa walimwonyesha vitambulisho vyao vikiwa na chapa ya serikali.

Hatimaye Kibatala alisimama na kumhoji kwa takriban saa moja. Kibatala, alimhoji shahidi huyo kwa nini yeye ndiye alikuwa wa kwanza kushuhudia tukio la kukamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi kwa vijana hao wakati mbele ya sehemu yake ya biashara kulikuwa na fremu zingine za biashara na kulikuwa na watu waliokuwa wakiendelea na kazi.

Kibatala pia alimbana shahidi huyo aeleze kama ni shahidi wa uongo au la, kwa kile alichodai kuwa maelezo yake ya ushahidi yaliyowasilishwa mahakamani yanapishana na kujichanganya mara kwa mara alipohojiwa na mawakili tofauti.

Pia alimhoji Valerian, aliyejitambulisha kuwa ni mfanyabiashara wa mbege, endapo ana tatizo la kupoteza kumbukumbu, hivyo kujibu kwamba hana tatizo hilo licha ya kwamba kuna kusahau kibinadamu.

"Unasema walipopekuliwa mshtakiwa namba moja alikutwa na kitu kigumu kwenye mfuko wake wa kushoto wa suruali. Wewe ulihusika kumpekua?" alihoji Kibataka na shahidi huyo kujibu kwamba hakuhusika.

Baada ya jibu hilo, Kibatala aliendelea kuhoji: "Kama hukuhusika kwenye upekuzi, ulijuaje kwamba kitu hicho kwenye suruali kilikuwa kigumu?" Shahidi alijibu kuwa alijua ni kigumu baada ya kutolewa na kujua kwamba ni bastola.

"Umeiambia mahakama kwamba kitu kingine alichokutwa nacho ni kete za dawa za kulevya zikiwa zimefungwa kwenye nailoni. Zilikuwa kwenye hali ya kimiminika au kitu kigumu?" Alihoji Kibataka kisha shahidi kudai kuwa zilikuwa laini.

Pia Kibatala alimhoji kwamba shahidi alidai kuwa mshtakiwa alikutwa na bastola ikiwa na magazini na risasi na je, anaijua magazine? Shahidi akadai kwamba haijui.

Awali, akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Esther Martin, shahidi huyo alidai kuwa aliyedai kumtambua mshtakiwa namba moja, Mohammed Abdalah, na namba mbili, Adamu Kusekwa.

Valerian alidai kuwa Agosti 5, mwaka jana, akiwa katika eneo lake la biashara, wakati akifanya usafi, aliwaona vijana wawili waliokuwa katika kibaa baa ya jirani na ofisi yake wakinywa pombe na baadaye kwenda katika banda la kusajili laini za simu.

Aidai kuwa vijana hao wakiwa katika eneo hilo aliwaona wakiwa wanazungumza na simu mara kwa mara na baada ya muda mfupi walitokea askari polisi wawili na kuwaweka chini ya ulinzi wakiwatuhumu kwamba wanatuhumiwa kwa ugaidi.

Kesi hiyo itaendelea leo kwa shahidi namba tano wa Jamhuri.

HABARI KITAIFA

# Chanjo corona dozi 500,000 toka China zawasili

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imepokea dozi 500,000 za chanjo ya corona aina ya Sinopharm, kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ikiwa msaada unaotokana na ushirikiano bora baina ya nchi hizo mbili.

Shehena hiyo ilipokewa jana Dar es Salaam na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyeambatana na viongozi wengine wa kitaifa na mkoa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Dk. Gwajima aliipongeza China kwa ushirikiano inaoendelea kuonyesha ikiwa ni pamoja na kusaidia kuboresha sekta ya afya nchini katika mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo corona.

"Shukrani za pekee ziwaendee serikali ya China hususani katika kujali afya za Watanzania kwa kutupatia chanjo hizi aina ya Sinopharm dozi 500,000 ambazo zitatusaidia kuwakinga Watanzania 250,000 dhidi ya mapambano ya ugonjwa wa UVIKO-19 (corona)," alisema Dk. Gwajima.

Alisisitiza kuwa China inathamini afya za Watanzania ndiyo maana imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma za kinga nchini.

Pia alisema serikali ilipata chanjo dozi 1,058,400 aina ya Janssen (Johnson and Johnson) ambazo zilishaisha na Sinopharm Dozi 1,065,600 zinazoendelea kutolewa katika vituo vyote nchini na kupitia huduma ya mkoba.

Aidha, Dk. Gwajima alisema, wizara ilitoa mwongozo wa chanjo unaofafanua vyema taratibu za utoaji wa chanjo hizo wenye lengo la kufikia uchanjaji wa asilimia 60 ya Watanzania wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

"Wizara ilitoa mwongozo wa chanjo unaofafanua vyema taratibu za utoaji wa chanjo hizi wenye lengo la kufikia uchanjaji wa asilimia 60 ya Watanzania wenye umri wa miaka 18 na kuendelea," alisisitiza.

Pia Dk. Gwajima aliipongeza mikoa mitano ambayo inaongoza kwa kasi ya utoaji wa chanjo ya Sinopharm ambayo ni Ruvuma, Mbeya, Mtwara, Dodoma na Kagera.

Dk. Gwajima alioa wito kwa jamii nzima kujitokeza kupata chanjo hiyo dhidi ya UVIKO-19, ili kupunguza milipuko ambayo inaweza kutokea mara kwa mara na kuepuka madhara makubwa kama kifo na kulazwa kwenye oksijeni kwa muda mrefu.

Sambamba na hilo, aliwaomba wadau wote wenye nia ya kusaidia eneo hilo la huduma ya chanjo kujitokeza na kufuata utaratibu wa mwongozo wa serikali ili kutoa msaada huo.

# EWURA kuanza msako vituo bubu mafuta

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatarajia kuanza msako kubaini wafanyabiashara wanaouza mafuta ya taa, dizeli na petroli bila leseni.

Lengo la msako huo, kwa mujibu wa NEMC, ni kudhibiti matukio ya moto yanayoweza kutokea maeneo mbalimbali.

Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, alisema hayo jana wakati wa kikao kazi kati ya wadau wa nishati na viongozi wa Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga. Wadau hao walikutana ili kujadili namna bora ya kutatua kero zilizopo katika sekta ya mafuta na gesi ambayo imekuwa ikiripotiwa na wananchi.

Alisema mikoa ya kanda ya ziwa inaongoza kwa matukio ya nyumba kuwaka moto unaosababishwa na uhifadhi wa mafuta ya petroli na dizeli kwenye makazi ya watu.

"Tutaendesha msako katika mikoa wa Shinyanga na Geita ili kuwabaini wafanyabiashara wote wanaouza mafuta kwenye chupa za maji mbele ya nyumba na maduka yao ya biashara.

Mhina alisema kuuza nishati hiyo bila utaratibu ni kinyume cha maelekezo ya EWURA na kuwataka wajisalimishe wenyewe kabla msako haujaanza," alisema Mhina.

"Mafuta ni kiminimika hatari ambacho huhifadhiwa kwenye matangi yanayochimbiwa ardhini, lakini wafanyabiashara wadogo wanauza mafuta kwenye chupa za maji ya kunywa kwa kuziweka nje juani hali ambayo inaweza kusababisha milipuko na kuyafanya yakose ubora pindi yanapotumiwa kwenye vyombo vya moto.

Alisema EWURA inatoa leseni kwa wafanyabiashara wanaomiliki vituo vya mafuta waliokidhi vigezo vya kisheria, lakini kwa wale wanaouza kwenye mapipa, madumu na chupa za maji hususani maeneo ya vijijini hao ndiyo hawatakiwi kwa mujibu wa sheria.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Wilfred Edwin, alisema kwa sasa kuna utaratibu unaowataka wamiliki wa vituo vya mafuta vilivyoko mijini kujenga vituo vingine hususani vijijini ili kudhibiti wimbi la wauzaji wa mafuta wasio na leseni.

Alisema uwekaji wa vinasaba katika mafuta ya taa, petroli na dizeli kabla ya kuingia sokoni umesaidia kupunguza uchakachuaji wa nishati hiyo kwa asilimia 80 na kupunguza malalamiko yaliyokuwa yanawasilishwa EWURA kuwa mafuta ni machafu.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo wa Benki ya NBC, Raymond Urassa (kulia), akiongea na waandishi wa habari (hawapo pichani) kabla ya kuendesha droo ya kutafuta washindi wa promosheni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani' inayolenga kuwahamasisha wakulima wa zao la korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara, waweze kujiunga na akaunti ya NBC Shambani iliyofanyika makao makuu ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam, jana. Wengine ni maofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Jorum Mtafya (katikati) na Neema Tatock. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge la 12 kuanza leo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MKUTANO wa Tano wa Bunge la 12 unatarajia kuanza vikao vyake leo huku miongoni mwa shughuli zitakazofanyika ni pamoja na wabunge kujadili na kuishauri serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge ya 94(1), katika mkutano wake wa Oktoba-Novemba kwa kila mwaka, Bunge kwa siku zisizopungua tano litakaa kama Kamati ya Mipango ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 63(3)(C) ya Katiba kwa kujadili na kuishauri serikali kuhusu mapendekezo hayo.

Katika mkutano huo, Bunge pamoja na mambo mengine litapokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali.

Aidha, kwa mujibu wa kanuni ya 94 (2) (b) pia Bunge litapokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato vya serikali na (C) litapokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa mpango wa serikali na vipaumbele kuhusu mpango huo.

Ratiba inaonyesha kuwa wabunge watapokea maelezo kuhusu maeneo ya vipaumbele vya matumizi ya fedha za mkopo nafuu zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF), kwa ajili ya kukabiliana na athari za Uviko-19.

Pia Bunge litapokea maelezo kuhusu miradi ya nishati ya umeme ya kimkakati na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake na taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo.


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

*Kwa Idhini tuliyopewa* na ***BANK OF AFRICA*** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba pamoja na gharama za dalali. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | **WANTANSHI LOUNGE** | Nyumba ya makazi yenye Hati na.23659 Kiwanja na.1318 Ofisi ya ardhi na.39847 iliyopo Msasani Peninsular | 15/11/2021 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor**
**P.O. BOX 1088**
**Dar Es Salaam.**
**Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, Ohio street/kivukoni**
**P.O. BOX 3054,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255-22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

216547502

# AZAKI zatoa neno kufukuliwa kaburi la mwili mwenye ualbino

**Na Thobias Mwanakatwe**

WANAHARAKATI na watetezi wa haki za binadamu wameibuka na kulaani kitendo cha kufukuliwa kwa kaburi la mtu mwenye ualbino, Heri Kijangwa, na kunyofoa mguu kisha kutoweka nao.

Wanaharakati hao, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), licha ya kulaani kitendo hicho, wametaka msako dhidi ya waliohusika pamoja na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, akisoma taarifa kwa niaba ya THRDC na TAS jana mbele ya waandishi wa habari, alisema kitendo hicho ni kosa la jinai, hivyo watuhumiwa wasakwe na kufikishwa mahakamani na adhabu kali itolewe ili iwe fundisho kwa wengine wenye nia ya kufanya vitendo vya uvunjifu wa sheria na haki za binadamu.

"Tunafahamu tukio hili limeripotiwa kwenye Kituo cha Polisi Bumbuli wilayani Lushoto mkoani Tanga. Tunahimiza serikali na Jeshi la Polisi kuhakikisha kesi hii haitaishia kwenye ngazi ya upelelezi badala yake watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani," alisema.

Henga alisema katika kipindi cha miaka minne iliyopita, matukio hayo yalikoma kabisa kutokana na jitihada za serikali kwa kushirikiana na wananchi na vyombo vya habari.

"Kwa masikitiko makubwa LHRC, TAS na THRDC tunalaani vikali vitendo hivi vya kikatili na vya kinyama vinavyotweza utu wa binadamu na vya kudhalilisha maiti," alisema.

Aliongeza kuwa matukio hayo yanavunja haki, utu na heshima ya binadamu kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu na sheria za nchi kama vile Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 (marejeo ya 2019).

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na mfululizo wa matukio hayo, hofu, wasiwasi na shaka kwa watu wenye ualbino vimeanza kurudi kulinganisha na miaka iliyopita.

Heri Kijangwa (45) alifariki dunia Julai 4, 2020 kwa maradhi ya kansa ya ngozi na alizikwa Julai 7, mwaka jana katika kijiji cha Tanda, Lushoto mkoani Tanga. Hata hivyo, katika hali isiyo ya kawaida, Oktoba 24, mwaka huu, watu wasiojulikana walifukua kaburi la marehemu huyo na kunyofoa mguu wake wa kulia na kutoweka nao kusikojulikana.

Kwa mwaka huu, hilo ni tukio la pili kutokea la kwanza likiwa kati ya Mei 3 na 4 baada ya mwili wa mtoto mwenye ualbino mwenye umri wa miaka mitano, kuokotwa ukiwa umekatwa mikono yote miwili katika kijiji cha Nondo, Uyui mkoani Tabora.



Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wakiwa katika kikao kilichoongozwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kilichofanyika jana, ofisi za Bunge jijini Dodoma. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# NEMC yakiri ujenzi mabondeni tatizo sugu

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema ujenzi holela kwenye mabonde na mito bado ni tatizo kubwa linalosumbua hasa kwenye mkoa wa Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa mkutano wa watendaji kata na mitaa kuhusu Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kanuni zake.

Dk. Gwamaka alisema ujenzi holela umekuwa na madhara makubwa hasa wakati wa mvua, hivyo kusababisha mafuriko kufika kwenye makazi ya watu na kuharibu mali pamoja na kutishia usalama wa wakazi hao.

Mbali na ujenzi holela, alisema utupaji wa taka ovyo limekuwa tatizo kubwa kwenye mkoa wa Dar es Salaam kwa watu kuyageuza maeneo mbalimbali kuwa dampo.

"Wengi wenu mmeshuhudia sehemu kubwa ya mabonde yamegeuzwa madampo sasa hilo ni kosa kubwa kwa sababu taka hizo zinakwenda baharini sasa mtiririko wa sumu zote zinaliwa na samaki ambao mwisho tunawanunua pale Ferry, tunakula sisi binadamu jambo ambalo ni hatari kiafya," alisema Dk. Gwamaka.

Alitaja tatizo lingine kuwa ni uchimbaji holela wa mchanga kwenye mabonde na uchimbaji wa kokoto na vifusi maeneo nyeti kimazingira na kwamba ingawa NEMC imekuwa ikitoa elimu na kukataza, matendo hayo bado yanaendelea kwenye jamii.

Pia alisema ujenzi holela wa viwanda vidogo vidogo, baa, kumbi za starehe na nyumba za ibada kwenye makazi ya watu ni jambo ambalo linalosababisha kelele na malalamiko ya wananchi wanaoishi maeneo hayo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Rugwa, aliishukuru NEMC kwa kuandaa mafunzo hayo aliyosema ni muhimu kwa watendaji hao ambao kwenye maeneo yao ndiko kwenye viwanda.

Alisema suala la usimamizi wa mazingira ni suala nyeti linalohitaji ushirikiano wa pamoja kwani kuna umuhimu wa kurithisha mazingira mazuri kwa vizazi vilivyopo na vizazi vijavyo.

"Haya mazingira mazuri tunayofaidi leo hii ni matunda ya kazi kubwa iliyofanywa na wazazi wetu, tusifikiri kwamba yalitokea tu hapana kuna kazi kubwa ilifanywa ili tuwe na mazingira bora hivyo nasisi tuhakikishe tunawarithisha mazingira bora watoto wetu," alisema.

Alisema watendaji wa kata na mitaa ni wadau muhimu sana wa maendeleo kwa serikali kwani wakifanya vibaya mambo mengi yanaharibika na iwapo watafanya vizuri kila kitu kinakwenda sawa.

"Kuna usemi kwamba ukitaka kufika haraka nenda peke yako, lakini ukitaka kufika mbali nenda na wenzako ndiyo maana naishukuru NEMC kwa kutambua umuhimu wa usemi huu na kuona kwamba ili ifike mbali lazima iende na ninyi," alisema.

## Dola milioni 30 kutunza shoroba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imezindua mradi wa uhifadhi wa miaka mitano utakaogharimu dola za Marekani milioni 30.5 kukabiliana na uharibifu wa mapito ya wanyamapori, maarufu kama shoroba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Ubalozi wa Marekani nchini, mradi huo ujulikanao kwa jina la 'USAID Tuhifadhi Maliasili' unatekelezwa na Research Triangle Institute International, taasisi ya utafiti wa maendeleo ya kimataifa.

Taarifa hiyo ilisema lengo la mradi ni kuangalia mienendo inayotishia harakati za wanyamapori na uhifadhi wa muda mrefu wa baioanuwai nchini Tanzania.

"Katika miongo michache iliyopita, Tanzania imepoteza angalau theluthi moja ya mifumo ya ikolojia yake na kushuhudia idadi ya viumbe vilivyo hatarini kuongezeka mara tatu. Takriban asilimia 25 ya mapato ya nje yanatokana moja kwa moja na utalii ambao kwa sehemu kubwa hutegemea sekta ya uhifadhi wa wanyamapori," ilisema taarifa hiyo.

Pia taarifa hiyo ilisema kiwango cha sasa cha kupungua kwa 'species' (aina ya wanyamapori), athari kwenye uthabiti wa kiuchumi inatarajiwa kuwa kubwa siku zijazo.

"Kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, USAID Tuhifadhi Maliasili itashirikiana na serikali ya Tanzania, jamii za wenyeji na sekta binafsi kutatua changamoto hizo. Tuhifadhi Maliasili inanuia kuunda mazingira ambamo njia za harakati zitaboresha ubora wa maisha kwa siyo tu wanyamapori bali pia jamii zinazowazunguka," ilifafanua taarifa hiyo.

Fedha hizo, kwa mujibu wa taarifa hiyo, zitatumika kwenye mradi wa kuimarisha uwezo wa taasisi kwa wadau wa sekta ya umma na binafsi, kupitia kuongezeka kwa ushirikishwaji wa sekta binafsi, pia utaimarisha sera ya udhibiti na mazingira rafiki kwenye usimamizi wa maliasili.

"Kwa kasi ya sasa ya upungufu wa viumbe, Tanzania iko njiani kupoteza kiasi kikubwa cha utalii, ambacho kitakuwa na athari kubwa za kiuchumi," alisema Kate Somvongsiri, Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania.

"Ingawa hatuwezi kubadilisha uharibifu wa awali wa wanyamapori na maliasili, kuendelea, mradi wa USAID wa Tuhifadhi Maliasili utawezesha usimamizi endelevu katika ngazi ya jamii na kitaifa," aliongeza.

**Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Ubalozi wa Marekani nchini, mradi huo ujulikanao kwa jina la 'USAID Tuhifadhi Maliasili' unatekelezwa na Research Triangle Institute International, taasisi ya utafiti wa maendeleo ya kimataifa.**

HABARI KITAIFA

# Ziara ya Mwinyi yaleta neema ya maji

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

ZAIDI ya wakazi 170 wa Kijiji cha Mleteni, Shehia ya Kisiwani, Wilaya ya Wete, Pemba, wamepata huduma ya majisafi na salama kutokana na ziara ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, aliyoifanya hivi karibuni kisiwani hapa.

Kijiji hicho ambacho kilikuwa hakijawahi kutembelewa na kiongozi hata mmoja, kinakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo ukosefu wa maji safi na salama.

Wakati Dk. Mwinyi alipofanya ziara kisiwani Pemba, alifika katika kijiji hicho na kusikiliza kero zinazowakabili wakazi wake na kuahidi kupeleka huduma hiyo ambayo sasa imewafikia.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walisema kwa nyakato tofauti kwamba ujio wa Dk. Mwinyi katika kijiji chao umeanza kuzaa matunda kwa kuwa wameshafikishiwa huduma hiyo ambayo ilikuwa kilio chao cha muda mrefu.

Mmoja wa wanakijiji hao, Said Mohamed Rashid, alisema wanakabiliwa na matatizo ya huduma mbalimbali ingawa wameanza kupata matumaini baada ya kuona wameanza kufikishiwa huduma ya majisafi na salama.

"Tunamshukuru sana Dk. Mwinyi kwa kutujali na kuja kututembelea kujua changamoto zinazotukabili na kuanza kuzipatia ufumbuzi. Hili ni jambo la faraja kwetu," alisema.

Mwananchi mwingine, ambaye hakutaka kutaja jina lake litajwe, alisema wamefurahia kupata huduma hiyo kwa kuwa walikuwa wakipata wakati mgumu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mwalimu wa Kituo cha Tutu katika kijiji hicho, Bishara Mbarouk Hamad, mkazi wa Kisiwani, alisema ukosefu wa maji ulikuwa kikwazo kikubwa kwa wananchi wa kijiji hicho.

"Tulikuwa tunachota maji kwenye madimbwi. Kwa kweli ilikuwa si salama, lakini sasa kimechimbwa kisima na kuwekwa tangi. Sasa yanatusaidia hata sisi tunaosomesha pale," alisema.

Sheha wa Shehia ya Kisiwani, Shaaban Salim Mtwana, alisema wananchi hao wamepata huduma hiyo baada ya kufika Dk. Mwinyi na kusikiliza kero zao.

"Kwa kweli kile kijiji kiko nyuma sana maana kilikuwa hakina huduma za kijamii hata moja. Nilikuwa napigania sana ili wafikishiwe huduma na wao wajione ni miongozi mwa wanajamii. Tunamshukuru Rais wetu alisema apelekwe na tukampeleka," alisema sheha huyo.

Naye Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Suleiman Anas Massoud, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanya jitihada mbalimbali kuona wananchi wa kijiji hicho kunapata huduma ya majisafi na salama.

Alisema ingawa kijiji hicho hakijafikiwa na huduma ya umeme, wametumia umeme jua katika kuwafikishia huduma ya maji na kwa sasa ni toshelevu kwa mujibu wa idadi ya watu.

Dk. Mwinyi hivi karibuni alikuwa na ziara kisiwani Pemba na kutembelea maeneo mbalimbali ya miradi ya maendeleo, kutembelea kijiji cha Mleteni na wananchi wa maeneo mengine kwa lengo la kusikiliza kero zao na kuzipatia ufumbuzi.



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko akiongea na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), waliomtembelea ofisini kwake kwa ajili ya kuanza kufanya kampeni ya utoaji elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango kwa wafanyabiashara mkoani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ubalozi India kuelekeza nguvu utunzaji mazingira

**Na Romana Mallya**

UBALOZI wa India nchini Tanzania, katika kusherehekea miaka 75 ya uhuru imeunga mkono juhudi za serikali katika utunzaji mazingira kwa kupanda miti.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan, alisema lengo ni kuimarisha uhusiano wa nchi hizo.

Pia alisema sherehe hizo zinafanyika kwa kuhusisha matukio mbalimbali ikiwamo programu zinazoelezea maendeleo na historia pana ya watu wa nchi hiyo, utamaduni na mafanikio.

Kadhalika, alisema wameandaa mashindano mbalimbali, maonyesho ya kitamaduni, ujumbe wa viongozi mbalimbali, programu za kubadilishana uzoefu na mipango ya elimu na mafunzo.

Alisema kikundi kijulikanacho kama 'Baba Gorekhnath Gotipua Dance Association' chenye watu 12 kiliwasili nchini tangu Oktoba 27 na kutumbuiza Bagamoyo na kundi la Jambo na Vijambo pia lilitoa burudani.

Alisema sherehe hizo zinahusisha Watanzania ambao kupitia tamasha la Diwali wameonyesha namna wanavyocheza ngoma za nchini humo maarufu Bollywood.

# Wenye ulemavu macho wapata matibabu D'Salaam

**Na Mwandishi Wetu**

WATU 100 wenye ulemavu wa macho jijini Dar es Salaam, wamepatiwa huduma ya kupima, matibabu na vifaa tiba katika kambi maalumu ya kupima macho iliyofanyika jana kwenye kituo cha Jumuiya ya Maendeleo ya Waislamu Wasioona Tanzania (VIMDAT).

Kambi hiyo iliyolenga kupima macho, kutoa miwani na matibabu mengine ya macho kwa wenye ulemavu jijini Dar es Salaam, iliratibiwa na Klabu ya Lions kwa kushirikiana na kampuni ya kubashiri matokeo ya Meridian Bet.

Mwenyekiti wa VIMDAT, Salim Benedictor, alisema kambi ya macho iliyofanyika jana inawapa faraja waathirika ambao baadhi yao walipatiwa dawa, miwani na wengine kutakiwa kufanyiwa upasuaji mdogo ili kuwasaidia kuona kidogo.

Aman Maeda wa kitengo cha ustawi wa jamii wa Meridian Bet, aliyeambatana na viongozi wengine wa kampuni hiyo, alisema wameamua kushirikiana na Klabu ya Lions katika huduma hiyo.

"Kwetu kambi hii ni muhimu kwa kuwa inagusa mahitaji yao na wako ambao watafanyiwa upasuaji mdogo, hivyo nitoe wito kwa jamii kuendelea kuwasaidia wenzetu hawa ili kupunguziwa makali ya tatizo linalowakabili," alisema.

Mratibu wa kambi hiyo kutoka Lions Club, Rizwan Qadri, alisema watu 100 wameshiriki kwenye kambi hiyo ambayo ilianza kwa kuwapima na waliohitaji kupewa dawa au miwani walipatiwa.

"Waliobainika kuwa na matatizo makubwa zaidi tutawapeleka CCBRT na Muhimbili kwa mtibabu zaidi kwa kushirikiana na wenzetu wa Meridian Bet," alisema.

**"Kwetu kambi hii ni muhimu kwa kuwa inagusa mahitaji yao na wako ambao watafanyiwa upasuaji mdogo, hivyo nitoe wito kwa jamii kuendelea kuwasaidia wenzetu hawa ili kupunguziwa makali ya tatizo linalowakabili," alisema.**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Zianze juhudi kuhifadhi maji mvua kukabiliana na ukame

**MABADILIKO** ya tabianchi yanaleta athari katika nyanja karibu zote kuanzia uchumi hadi mazingira, athari zake hazikwepeki na kwa Tanzania uhaba wa maji, upepo, vimbunga na ukame ni masuala ambayo sasa ni bayana.

Licha ya kuwapo juhudi mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko hayo, changamoto bado ni kubwa na inapotokea uhaba wa mvua unaombatana na upepo mkali kama ilivyokuwa mwaka huu wananchi wanaathirika.

Miongoni mwa juhudi ambazo zimechukuliwa na serikali ni kuibua vyanzo vipya vya maji katika kukabiliana na upungufu wa huduma hiyo unaotokana na jua, upepo na ukosefu wa mvua kuathiri sekta ya maji.

Mkoani Dar es Salaam, juhudi za kuongeza maji kupitia mradi wa visima virefu vya Mpera na Kimbiji kufanikisha upatikanaji wa majisafi na salama kwa wakazi wa Kigamboni na maeneo mengine ya Temeke.

Kadhalika ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji la Kidunda mkoani Morogoro ikiwa ni sehemu ya juhudi za serikali za kuhakikisha yanakuwapo maji ya kutosha wakati wote bila kujali ni masika au kiangazi kwa watu wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Lakini shida ya maji bado haijaisha. Tunaona kuwa kazi zaidi na ubunifu unahitajika. Vyanzo vya maji vya Ruvu na Wami ambavyo hulisha Dar es Salaam na Pwani vimepungua, lakini kwa Tanzania nzima mabadiliko hayo, ukataji miti na uharibifu wa mazingira na kilimo na ufugaji kwenye maeneo jirani na mito yameendelea kuwa tishio kwa usalama na upatikanaji wa maji.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania TMA, imeshatoa mwelekeo wa hali ya mvua na kutaja uwepo wa vipindi virefu vya ukame kuanzia sasa hadi Januari mwakani yote haya yanatishia hatima ya maji nchini na kwa mazingira hayo ni wazi kuwa Mamlaka za Maji, Usafi wa Mazingira Mijini zina kazi kubwa kufikiria namna ya kumaliza changamoto ya maji mijini huku Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) nao ukitakiwa kubuni na kutekeleza mikakati ya kumaliza shida ya maji vijijini.

Kwa hali kama hiyo, tunaishauri serikali kuanza sasa kulifanyia kazi suala la kuhifadhi maji mengi ya mvua yanayopotea kila mwaka ili wananchi wasipate shida hasa nyakati za ukame.


Mvua zinazonyesha na hata kuwa juu ya viwango na mafuriko yanayotokea sehemu nyingine, yote hayo ni maji yanayopotea. Ndiyo maana tunaomba sasa serikali iamke na kuona namna bora ya kutunza mabilioni ya lita za maji ya mkvua yanayopotea kila mwaka kwa kuchimba mabwawa mengi zaidi na kuweka hifadhi za maji za taifa kwenye kanda, mikoa na wilaya.

Tunashauri zifanyike njia mbalimbali za uvunaji wa maji hayo ili yasipotee bure, bali yavunwe na kuhifadhiwa kwa ajili ya mahitaji ya baadaye badala ya kuacha yapotee kila mwaka huku wananchi wakikosa maji safi na salama.

Kwa mfano TMA inasema, kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini kinatarajiwa kupungua hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani.

Kutokana na mazingira kama hayo, ndiyo maana tunashauri kuongezwa kwa vyanzo vingi zaidi na kufanya juhudi za kuhifadhi maji, serikali iwekeze eneo hilo kwani uhaba huo unapelekea kuwepo magojwa na kuongeza gharama zaidi kwa serikali kwenye sekta ya afya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Faustine Feliciane

## Ni muhimu kujipanga kuelekea uhaba wa mvua

**VIASHIRIA** vya kuwepo mvua ndogo, za wastani mpaka chini ya kiwango kwa mikoa inayozalisha chakula kwa wingi, vinaongeza wasiwasi wa upungufu wa mavuno msimu huu wa mvua.

Mikoa inayoelekea kuathiriwa na hali hiyo ni Mbeya, Iringa, Njombe, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Lindi, Mtwara na baadhi ya maeneo ya magharibi ya mkoa wa Morogoro.

Lakini pia, uhaba umeonekana mikoa ya kanda ya kati, Dodoma na Singida na baadhi ya sehemu za mkoani Kigoma.

Hali hiyo inaonekana wakati msimu mpya wa mvua kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka ukitarajiwa kwa maeneo mengi kuanza mwezi huu na kuendelea hadi Aprili mwakani.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwenye utabiri wake wa msimu huu wa mvua, inabainisha kuwapo na viashiria vya uhaba wa mvua mpaka chini ya wastani kwa mikoa hiyo.

TMA inaeleza kuwa mikoa hiyo muhimu na vinara kwenye uzalishaji wa chakula nchini inaelekea kuathiriwa na uhaba huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TMA Dk. Agnes Kijazi, anayasema hayo wakati wa kuwasilisha utabiri hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

Maeneo hayo yamekuwa ni moyo wa kuzalisha chakula hapa nchini hivyo kuwepo kwa uhaba wa mvua ni jambo ambalo linalostahili kupewa uzito wa kipekee.

Kukosekana kwa mvua za kutosha TMA inatahadharisha kuwa kutasababisha kukosekana kwa unyevu unyevu kwenye udongo na hivyo na kukwamisha ukuaji wa mazao kikamilifu.

Ingawa bado serikali haijatoa tamko, kuna uwezekano wa mavuno ya kipindi hiki cha mvua yakawa pungufu na hata kusababisha upungufu wa chakula.

Hivyo basi ni vyema sasa kamati za maafa mikoa na wilaya, kata na kijiji kuanza kujipanga mapema na kuchukua hatua kukabiliana na upungufu huo wa mvua unaoweza kusababisha na kuongeza ugumu kwenye kilimo na upatikanaji wa chakula.

Yapo mabwawa ya asili ya kutunza maji lakini zipo skimu za umwagiliaji na njia nyingine za kuvuna maji, hivyo hata hayo madogo yakusanywe ili kusaidia kwenye kilimo husus ani kile kilimo cha umwagiliaji kwa baadhi ya maeneo nchini.

Lakini, wakulima ni vyema kuangalia mwenendo wa mvua na kupanda mazao ambayo yatastahimili ukame huku yakitumia mvua ndogo ili kujihakikishia chakula.

Wakulima wafuate ushauri wa wataalamu unaotolewa hususani maofisa ugani na kufuata maelekezo yao ili kuondokana na athari zozote ambazo zinaweza kutokea kwa ukosefu wa mvua unakotarajiwa.

Mazao kama mihogo, viazi, mtama, mbaazi na ufuta ni muhimu kulimwa katika kipindi hiki kutokana na ukweli kuwa mazao hayo yanastahimili mvua ndogo na ni mazao ya chakula.

Kwa Watanzania wakati TMA ikiendelea kutoa utabiri ambao imeugawa katika makundi tofauti ukianzia utabiri wa kila mwezi, wa siku tano pamoja na ule wa kila siku, wananchi wanapaswa kufuatilia taarifa zake, kuchukua tahadhari pale wanapopewa maelekezo. Lengo ni kuwa na mipango bora ya kilimo na maandalizi yenye tija ya kipindi kigumu cha upungufu wa mvu.

Lakini pamoja na hayo yote, hali kama hii iwakumbushe wadau mbalimbali kuwa na mikakati ya kujenga mabwawa ya kuhifadhia maji katika maeneo yanayowezekana ili kukabiliana na uhaba wa maji pale mvua zinapopungua au upepo kukausha vyanzo vya maji.

Mwaka huu umekuwa na upepo mkali ambao athari zake ni pamoja na kukausha maji mtoni, mabwawani na hata kwenye skimu za kilimo.

# Wazee waomba kasi katika usambazaji chanjo Corona

**Na Deogratius Nsokolo,**
KIGOMA

MTANDAO wa mashirika yanayohudumia wazee Tanzania, umeiomba serikali kuongeza kasi ya utoaji chanjo ya Uviko-19 kwa wazee hasa waliopo maeneo ya pembezoni na vijijini kutokana na wengi kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu ugonjwa huo na kutochukua uamuzi wa kuchanja.

Mwenyekiti wa mtandao huo, Kotilda Kokupima, alisema wakati wa kikao cha uhamasishaji katika Baraza la Wazee Wilaya ya Kasulu, pamoja na serikali kutoa kipaumbele kwa wazee kupatiwa chanjo ya ugonjwa wa corona, bado wengi hawajafikiwa na huduma kutokana na kutopata taarifa sahihi.

Kokupima ambaye ni Mwenyekiti wa Shirika la Wazee Mkoa wa Kigoma (EWAKI), alisema wazee wanakabiliwa na magonjwa mengi kutokana na umri wao ambao unaruhusu magonjwa kutokana na kushuka kwa kinga ya mwili na kusisitiza ni muhimu wakafikishiwa huduma majumbani kwa kuwa wengi hawana uwezo wa kufuata katika vituo vya kutolea huduma.

Mmoja wa wazee katika mkutano huo, Alberto Mungerere, aliamua kuchanja alisema kunahitajika kuwapo kwa mkakati maalum wa kuwanusuru wazee kwa sababu wako hatarini zaidi kuambukizwa, pia hawana elimu ya kutosha kuhusu manufaa ya chanjo hiyo.

Kwa upande wake, Meneja Programu wa Shirika la Iisilo la kiserikali Help age Tanzania, Joseph Mbasha, alisema kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), wanaendesha mpango wa elimu kwa wazee katika mikoa ya Kigoma na Mwanza ili kuwawezesha kupata elimu na chanjo.

Alisema wamelenga kuhakikisha wanachangia ongezeko la wazee kupata chanjo kwa kuunga mkono jitihada za serikali na wadau wengine na katika Mkoa wa Kigoma na wanatarajia kuwafikia wazee 300.

Alisema wanafanya mikutano na wazee kupitia mabaraza ya wazee ya wilaya ambayo yanaundwa na wao kutoka kila kata na wataalam wa afya wanatoa elimu na chanjo kwa wenye hiari kuchanjwa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwakinga wazee na ugonjwa wa Uviko-19.

Ofisa Ustawi wa Jamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Salum Masaga, alisema kazi kubwa inayofanywa sasa ni kuhakikisha wazee wanapata elimu sahihi na chanjo kwa kuwa ni haki yao na halmashauri hiyo imeweka mazingira mazuri ya kuhakikisha zoezi hilo linafanikiwa.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya siku moja kuhusu masuala ya huduma za fedha kwa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari yaliyofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanahabari waombwa kutoa elimu ya fedha

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

SERIKALI imeviomba vyombo vya habari kusaidia kuwaelisha wananchi kuhusu uelewa wa masuala ya kifedha ili kukuza uchumi.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alitoa wito huo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja kwa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini.

Tutuba aliviomba vyombo vya habari nchini kulisaidia taifa katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya huduma za kifedha kwa kuwa taarifa zao kufuatiliwa na jamii kila siku.

"Tumeona tuwajengee uwezo wa uelewa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini ili kutoa elimu kwa wananchi wetu kuhusu masuala ya kifedha kwa sababu wanafuatilia taarifa zenu kila siku," alisema.

Alibainisha kuwa mafunzo hayo ya siku moja yalikuwa na lengo la kuwajengea uelewa wa masuala muhimu yanayohusu sekta ya huduma za fedha ili kuisaidia jamii.

Tutuba alisema kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kuelimisha umma, wizara iliona ni vyema kutoa mafunzo yao kwa wahariri ili elimu iweze kuwafikia wananchi.

Katibu mkuu huyo alisema Wizara ya Fedha na Mipango ina lengo la kutatua tatizo za uelewa wa wanachi kuhusu masuala hayo ya kifedha ili wajikwamue kiuchumi.

Aidha, Tutuba alisema wizara hiyo imeandaa maadhimisho ya wiki ya huduma za fedha kitaifa yatakayofanyika kuanzia Novemba 8 hadi 14, mwaka huu, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Alisema katika wiki hiyo wanatarajia kujielekeza katika masuala ya kujenga weledi na uelewa umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma za fedha na kuimarisha ufanisi wa masoko ya fedha .

# AZAKI zakumbushwa uwajibikaji utendaji kazi

**Na Romana Mallya**

MGANGA Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, amezitaka asasi za kiraia kufanya kazi kwa kuzingatia uwajibikaji, uwazi na nidhamu kwenye matumizi ya fedha zinazotolewa na wadau wa maendeleo.

Aliyasema hayo juzi wakati akizindua mpango mkakati wa miaka mitano wa Taasisi inayojihusisha na kuhamasisha afya Tanzania Health Promotion Support (THPS).

Pia Dk. Sichwele alitaka kutengenezwe mpango mkakati utakaowezesha taasisi hizo kupata fedha bila kutegemea ufadhili.

Mkurugenzi Mtendaji wa THTS, Dk. Redempta Mbatia, alitaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo miaka 10 iliyopita kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa eneo ambalo taasisi hiyo inatoa huduma zake.

"Taasisi hii pia imewezesha kupatikana kwa watumishi wa afya wapatao 793 wanaofanya kazi kwa mkataba katika vituo mbalimbali nchini," alisema.

Alisema wametumia zaidi ya Sh. bilioni 7.3 kununua vifaa mbalimbali vya tiba vinavyotumika kuwasaidia Watanzania.

Wanufaika wengine ni katika maeneo ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi, kifua kikuu na tiba yake, afya za mama na uzazi pamoja na mapambano ya ugonjwa wa UVIKO.

Dk. Mbatia alisema mpango mkakati mpya wa THTS umelenga kuongeza uwezo wa taasisi ili itimize majukumu yake kwa ufanisi na kuongeza nguvu katika utawala bora katika matumizi ya fedha, rasilimali watu, manunuzi na mifumo ya Teknolojia ya Mawasiliano kwa kipindi cha mpango huo kuanzia 2021 hadi mwaka 2025.

Aidha, alisema vipaumbele vya mpango huo wa miaka mitano ni kuongeza uwezo wa taasisi, utoaji wa huduma za afya, kuboresha huduma za afya na ufuatliaji na tathmini.

Alisema taasisi itaendelea kuimarisha uwezo wake katika kutoa huduma bora za afya, mifumo ya fedha taarifa za uongozi, manunuzi rasilimali watu pamoja na mifumo mingine ya uendeshaji.

# Mkuranga yauza tani milioni 1.3 korosho

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAKULIMA wa korosho wilayani Mkuranga mkoani Pwani, wameuza tani milioni 1.3 ya zao hilo katika mnada wa pili wa mfumo wa stakabadhi ghalani uliofanyika wilayani hapo.

Akizungumza na wakulima hao kutoka Vyama vya Msingi AMCOS, Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORRECU), Hamis Mantawale, alisema wazabuni 13 walijitokeza.

"Katika mnada wa uuzwaji wa korosho wazabuni 14 walijitokeza kununua zao hilo," alisema.

Aidha, katika uuzwaji korosho kulikuwa na bei ya ununuzi kwa daraja la kwanza kilo moja iliuzwa kwa Sh. 2,500.62 huku daraja l a pili ikiuzwa kwa Sh. 1,673.10.

Alisema wanunuzi wote walionunua korosho hizo wanatakiwa kuingiza pesa ndani ya siku nne kabla ya kupeleka malipo AMCOS kupitia benki.

Mwakilishi wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Jafar Nataka, alimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkuranga, Mwantumu Mgonja, kwa kununua mzani na mikasi ya AMCOS kama ilivyopendekezwa katika kikao cha wadau wa korosho mkoani humo huku halmashauri zingine zikitakiwa kuiga mfumo huo.

Wakati huo huo, CORECU inatarajia kuandaa mafunzo kwa wawakilishi wa AMCOS ili wajue matumizi yake hatimaye korosho za mkoa huo ziongeze ubora.

Rashid Serungwi, Diwani wa Kata ya Mbezi Mkuranga, aliomba kiitishwe kikao cha wadau wa korosho haraka ili kizungumzie kushuka kwa bei ya korosho na kupungua kwa ubora wa zao hilo zikiwa ghalani.



Kampuni ya SUMA JKT wakifanya usafi sehemu za wafanyabiashara waliotoa vibanda vyao katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima waiangukia serikali

**Na Elizabeth John,** MBEYA

WAKULIMA 3,800 wa mpunga kutoka Bonde la Mnazi lililoko wilayani Mbarali, mkoani Mbeya wameiomba serikali kuangalia namna bora ya kutatua mgogoro wa ardhi baina yao na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Ombi hilo limetolewa hivi karibuni na wakulima wanaotumia eneo hilo wakiwamo umoja wa nguvu kazi Mwanavala, ambao wamekuwa na wasiwasi na kauli ya serikali kuhusu kufanya mapitio upya ya GN namba 28 inayohusisha vijiji 31 vilivyopo wilayani Mbarali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwa niaba ya wenzao, Upendo Kyambiki na Shabani Nguluvala, walisema kwa miaka mingi wanalima mpunga kwenye bonde hilo, na kwamba kutaka kuwaondoa jirani na eneo la Ihefu kutasababisha kushindwe kumudu maisha yao. Walisema wanategemea kilimo kwa shughuli zao za kujiingizia kipato cha familia na kwamba wakiondolewa eneo hilo watakosa pa kwenda na taarifa aliyopelekewa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa wako wachache sio za kujenga bali kuwaumiza.

"Sisi tumezaliwa Mbarali maisha yetu yote ni hapa hata makaburi ya ndugu zetu yapo hapa sasa tukifukuzwa tutaenda kuishi wapi tunaomba Rais asikie kilio chetu," alisema Upendo.

Naye Irene Ngailo, aliiomba serikali kuangalia namna bora ili wakulima waweze kuwa salama sambamba na kuendelea na kilimo hicho.

Mmoja wa viongozi wa umoja wa wakulima wa zao la mpunga wilayani Mbarali, Athanasi Kikwembe, alisema walipeleka rasimu inayoonyesha mahitaji ya mkopo wa fedha ya Sh. bilioni 3.1 kupitia eneo hilo sasa kitendo cha kutaka kuwaondoa kwenye eneo hilo ni kutowatakia mema.

Akizungumza kwa njia ya simu, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema alikwenda mkoani Mbeya ili kutembelea maeneo yote ya mkoa huo ambayo yana mwingiliano na maeneo ya hifadhi.

Alisema kulingana na maagizo ya Rais wameunda timu ya kufanya tathmini ambayo haitoleta taharuki kwa wananchi kwa kuzingatia maslahi mapana ya taifa.

# RC ataka elimu kwa watendaji wa mizani

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), kuwajengea uwezo watendaji wa mizani yote nchini ili kutoa huduma bora kwa wadau wa usafirishaji.

Homera aliyasema hayo jana wakati akifungua semina ya mafunzo ya siku moja kwa wadau wa usafirishaji kuhusu Sheria ya Udhibiti Uzito wa Magari ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2018 katika ukumbi wa BEACO jijini hapa.

"Elimu hii ya Sheria ya Udhibiti Uzito wa Magari ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2018, itolewe pia kwa watendaji wote wa TANROADS walio kwenye vituo vyote vya mizani nchini ili iwe rahisi kwao kuendelea kuwaelimisha wadau wa usafirishaji wanaotumia huduma za mizani nchini.

"Serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu bora ya barabara za mikoa, mijini na vijijini, hivyo ni jukumu la kila Mtanzania kulinda na kusimamia matumizi bora na sahihi ya miundombinu ya barabara nchini kwa maendeleo ya taifa letu", alisema Homera.

Mkuu huyo wa mkoa aliongeza kuwa msukumo wa mafunzo hayo unatokana na ukweli kuwa, wadau wengi wa usafirishaji nchini hawana uelewa wa kutosha juu ya sheria hiyo ya udhibiti uzito wa magari inayotumiwa na nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa Homera, hali hiyo inasababisha changamoto za mara kwa mara hasa inapotokea chombo cha usafiri kinapopimwa na mizani ya TANROADS na kukutwa kimezidisha uzito, hivyo elimu hiyo itasaidia kuondoa changamoto hizo.

Awali, Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Peter Mkolwa, alisema kuwa mafunzo hayo ni mwendelezo wa utoaji elimu ya Sheria ya Udhibiti Uzito wa Magari ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2018 ambayo yamekuwa yakitolewa kwa wadau wa usafiri wa barabara nchini tangu mwaka 2018 kabla ya kuanza kutumika rasmi kwa sheria hiyo Machi, 2019.

Nao wadau wa usafirishaji jijini Mbeya wanaohudhuria mafunzo hayo, wameitaka serikali kutilia mkazo upatikanaji wa elimu hiyo, kwa kuandaa mabango na vipeperushi mbalimbali ambavyo vitawaongezea uelewa juu ya sheria hiyo ya udhibiti wa uzito wa magari kwa kuwa kwa kufanya hivyo, wataepukana na makosa wanayoyafanya mara kwa mara kwa sababu ya kukosa uelewa.

# TAKUKURU kupambana wapenda rushwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, amewaonya wanaojihusisha na rushwa kwenye miradi ya maendeleo kuacha mara moja.

Suzana alitoa onyo hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari na kutoa taarifa ya miezi mitatu ya utendaji kazi wa taasisi hiyo.

Alisema TAKUKURU itakuwa macho muda wote kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezeka kwa kiwango kinachotakiwa kwa kuwa ndiyo njia sahihi ya kumsaidia mwananchi kupata huduma za kijamii.

"Tutahakikisha ukaguzi wa miradi unafanyika kila wakati kuwabaini wote wenye lengo ovu, niwaombe wana Pwani msisite kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwenye miradi ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria kwa wakati," alisema.

Alisema TAKUKURU itaendelea kufuatilia fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa lengo la kudhibiti ubadhirifu na pale itakapobainika wahusika watachukuliwa hatua.

Alisema taasisi hiyo itaendelea kuelimisha umma kuhusu madhara ili waifahamu nafasi yao katika mapambano dhidi ya rushwa ni ya Watanzania wote.

Suzana pia alisema utafanyika utafiti katika vyuo vilivyopo kwenye mkoa huo kuona visababishi vya rushwa ya ngono.

Alisema wataendelea kuanzisha klabu za wapinga rushwa shuleni ili elimu hiyo ianzie ngazi za chini na kuandaa kizazi kinachopambana na vitendo hivyo.

# Siku ya Mapacha kufanyika Dar

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Eden Twins Foundation linatarajiwa kufanya tamasha la Siku ya Watoto Mapacha, kama njia mojawapo ya kuhamasisha jamii kuwatambua na kuwahudumia kikamilifu.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa shirika hilo, Diana Joy Mbena, kwenye ofisi za gazeti hili, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana, kuelezea tamasha hilo litakalofanyika Novemba 11, mwaka huu.

"Eden Twins Foundation ni shirika jipya ambalo linajikita kuhudumia watoto mapacha, kwa kuwa wengi wao wanatoka katika familia duni na wanakumbana na changamoto nyingi katika maisha yao," alisema Diana.

Alisema, katika tamasha hilo shirika lake linajiandaa kuonyesha jamii jinsi baadhi ya familia zenye watoto mapacha zinavyohangaika ili mwisho wa siku zifanyike jitihada za kusaidia familia za aina hiyo.

"Karibu familia nyingi zenye watoto mapacha ni zile ambazo zina maisha duni, ndiyo maana nikaamua kuanzisha shirika hili, kwa lengo la kutaka jamii izitambue na kuzisaidia kwa hali na mali," alisema.

Diana alifafanua kuwa baadhi ya familia zenye mapacha, hazina uwezo wa kuwahudumia kwa chakula, matibabu na elimu, na kwamba taasisi hiyo inataka kutangaza vikwazo hivyo vijulikane.

"Wito wangu kwa Watanzania wajitokeze kwa wingi Novemba 11 kwenye viwanja wa TTCL Kijitonyama, ili kushuhudia tamasha la kutambua watoto mapacha na kuweka mikakati ya kuwasaidia," alisema.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoani Arusha, Mhandisi Reginald Massawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 3/- kila mwezi kuboresha mabomba chakavu

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira wilayani Bukoba mkoani Kagera (BUWASA), imetenga Shilingi milioni tatu kila mwezi kutoka makusanyo ya ndani kwa ajili ya kubadili miundombinu ya mabomba chakavu ili kuokoa upotevu wa maji.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Ofisa Matengenezo na Usambazaji wa Mtandao wa Maji, Kuboja Charles, alisema hatua hiyo itasaidia kupokea taarifa za kupasuka mabomba na kubaini upotevu wa maji yanayozalishwa kutoka chanzo kikuu.

Alisema shughuli hiyo inafanyika kwenye maeneo ya huduma na kwamba BUWASA ilitenga kanda tatu ambazo ni Kashai, mjini kati na ukanda wa juu.

Charles alisema kabla ya kuanza kubadili mabomba hayo timu ya mafundi ilitembelea mitaa hiyo na kubaini upotevu wa maji kwa asilimia 47 hadi 49 yanayozalishwa kwa mwezi.

"Tumebaini upotevu wa maji unasababishwa na uchakavu wa mabomba yanayopasuka kwa kuwa wateja walikuwa wanajiwekea wenyewe mabomba hayo waliyokuwa wakiyanunua dukani bila kujali ubora," alisema Charles.

Diwani wa Kata ya Kashai, Ramadhan Kambuga, alisema kuna matatizo ya maji yanayowakumba wakazi walio kwenye mitaa mbalimbali ndani ya kata hiyo.

Pia, alisema hali hiyo hulazimu kutafuta maji kwenye vyanzo vinavyotiririsha maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Katika kutatua tatizo hilo alianzisha mpango wa kufanya maboresho kwa kujenga ukuta katika chanzo hicho.

"Hatua niliyoifanya kwa wakazi niliitisha mkutano na kuonyesha mfano wa kujitoa kuchangia shughuli za maendeleo kwa kutoa Sh. 150,000 ambazo zilipangiwa kununua saruji na kulipa fundi ili waendelee kupata huduma," alisema Kambuga.

Alisema kupitia vikao vya kata ilipendekezwa kuomba wataalamu kutoka (BUWASA), kwa ajili ya kushughulikia tatizo la uchakavu wa mabomba hayo.

# ASA kuanza usambazaji wa mbegu za mpunga CHAURU

**Na Julieth Mkireri,** RUVU

WAKALA wa mbegu za kilimo Tanzania (ASA), wamesema wana mpango wa kuanza kusambaza mbegu za mpunga kwa Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU) kwa msimu wa kilimo utakaoanza hivi karibuni.

Hayo yamebainishwa juzi na msaidizi wa masoko wa ASA, Josephat Masanja, alipokuwa akizungumza na Nipashe kwenye maadhimisho ya Wiki ya CHAURU yaliyomalizika mwishoni mwa wiki.

Masanja alisema kabla ya kusambaza mbegu hizo wataanza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mbegu wanazozalisha.

Alisema mpango huo ni kati ya mikakati waliyojiwekea kuongeza usambazaji wa mbegu wanazozalisha katika maeneo mbalimbali nchini.

Kadhalika, alisema ASA wana mpango wa kuongeza uzalishaji wa mbegu za soya kutokana na uhitaji mkuu uliopo sasa pamoja na mbegu za alizeti.

"Mpango wetu ni kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti mahitaji yake yamekuwa makubwa hasa kwa Kanda ya Kati ambapo wakulima wameongezeka na mbegu za soya ambazo uhitaji wake umekua mkubwa mpaka nchi za nje kama China," alisema.

Alisema wana vituo 13 vya uzalishaji wa mbegu kupitia mashamba darasa ambayo wakulima wanajifunzia kuhusu mbegu bora kabla ya kusambaziwa.

"Mawakala wamekuwa wakisisitiziwa kuwa na mashamba darasa ili wakulima wajionee ubora wa mbegu na kuagiza, na kwa hapa nchini tuna mawakala 56 ambao wanasambaza mbegu katika maeneo mbalimbali," alieleza.

Akifunga maadhimisho hayo ya Wiki ya CHAURU, Mrajisi wa Mkoa wa Pwani, Anjela Nalimi, alitoa rai kwa viongozi wa ushirika huo kuhakikisha wanateketeza mazalia shambani ili muda wa kilimo unapoanza yasiwapo kuepusha wimbi la ndege waharifu wa mpunga.

Meneja wa CHAURU, Victoria Olotu, akisoma taarifa ya ushirika huo alisema ubovu wa miundombinu kwenye mashamba unapunguza uzalishaji kwa asilimia 40.

Katika taarifa yake meneja huyo aliiomba serikali kusaidia ukarabati wa barabara kutoka makao makuu ya CHAURU hadi barabara kuu ambayo inahitaji Sh. milioni 100 ili wakulima waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi kwa kipindi chote.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, akiwa na Kamati ya Ulinzi Mkoa katika Wilaya ya Songea wakitoka kukagua chanzo cha maji kijiji cha Liula kilichoko Mahilo Manispaa ya Songea. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# Wazazi wakumbushwa jukumu la malezi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZAZI na walezi mkoani Shinyanga, wamekumbushwa wajibu wa kuwalea watoto wao waliohitimu elimu ya msingi na kidato cha nne, pamoja na kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili ikiwamo mimba za utotoni. Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Boniphace Chambi, alibainisha hayo juzi kwenye mahafali ya 23 ya kidato cha nne, Shule ya Sekondari Don Bosco wilayani humo.

Alisema kipindi wanafunzi wanapokuwa likizo hujitawala na kufanya mambo yao wenyewe, huku wazazi wakiwa bize na maisha, kusahau wajibu wao wa malezi na kusababisha wanafunzi kuingia katika makundi mabaya, na wengine kupata ujauzito.

"Sasa hivi wanafunzi waliohitimu elimu ya msingi na kidato cha nne wapo nyumbani, jukumu la malezi ni la wazazi ili kuhakikisha watoto wanabaki salama na kuendelea kutimiza ndoto zao," alisema Chambi.

Alitoa mfano kipindi cha likizo ya corona, wazazi walisahau majukumu yao ya malezi na kusababisha wanafunzi wengi mkoani humo kupata ujauzito na wengine kuolewa ndoa za utotoni na kuzima ndoto zao za elimu.

Katika hatua nyingine, Chambi aliwataka wahitimu walio majumbani kwa sasa, wajilinde na kuacha kujiingiza kwenye makundi mabaya, pamoja na kutoa taarifa za ukatili, wakiwamo na wazazi wanaotaka kuwaozesha ndoa za utotoni.

Kwa upande wake Mkuu wa Shule ya Sekondari Don Bosco, Felix Wagi, akisoma taarifa ya shule hiyo, alisema wanafunzi waliohitimu kidato cha nne wapo 164 kati ya hao wasichana ni 67.

# RC Ruvuma aagiza vyanzo vya maji kulindwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, amekagua vyanzo vya maji kwenye miradi ya Ndongosi na Liula, wilayani Songea na kuagiza vyanzo hivyo kulindwa ili viwe endelevu.

Brigedia Jenerali Ibuge amesikitishwa na uharibifu wa vyanzo hivyo unaoendelea kufanywa na wananchi kwa kulima mazao na shughuli nyingine za kibinadamu hali inayosababisha vyanzo hivyo kuwa katika hatari ya kutoweka.

"Naagiza kila kijiji kuitisha mkutano mkuu wa kijiji, kati ya ajenda zake kuu, iwe ni namna gani ya kukabiliana na tabia hii ya kuharibu vyanzo vya maji, nimeona miti inavyoangushwa kama haina mwenyewe," alisema.

Alisema serikali inapenda watu wajipatie kipato kutokana na kilimo na ametahadharisha kuwa shughuli za kibinadamu ndizo zinazoathiri vyanzo hivyo.

Alitoa rai kwa wataalamu wote wa maji wakiwamo RUWASA na Bonde la Maji la Ziwa Nyasa, waende vijijini ili kutoa elimu ya mazingira kwa wananchi na kuweka ramani kwenye eneo zima lenye vyanzo vya maji na kuagiza utekelezaji wa maagizo hayo ufanyike kabla ya Desemba Mosi, mwaka huu.

"Tusiseme tuna changamoto ya tabianchi ni sisi wenyewe ndiyo tunaoharibu kwa kukata miti, kulima hadi kwenye kingo za mito, tunachoma moto misitu na kuvunja sheria mbalimbali za mazingira," alisema RC Ibuge.

Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji ya kijiji cha Ndongosi na Liula kwa Mkuu wa Mkoa, Meneja RUWASA Wilaya ya Songea Mhandisi, Mathias Charles, alisema mradi wa maji Ndongosi ulisanifiwa kwa zaidi ya Sh. milioni 332.

Hata hivyo, alisema kati ya fedha hizo zaidi ya Sh. milioni 23 ni fedha za maandalizi ya mradi, zaidi ya Sh. milioni 51 ni za usimamizi na zaidi ya Sh. milioni 256 ni fedha za ujenzi wa mradi wa maji.

Aliutaja mradi wa maji Ndongosi kuwa ulisanifiwa kuhudumia wakazi 3,175 wenye mahitaji ya maji lita 119,062.5 kwa siku na chanzo kutoka Mto Mlaimonga kina uwezo wa kuzalisha maji lita 902,016 kwa siku na kwamba mradi umefikia asilimia 98.

Kuhusu mradi wa maji wa kijiji cha Liula, mhandisi huyo alisema mradi huo awali ulisanifiwa kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni moja na RUWASA kwa kutumia wataalamu wake wa ndani wamefanikiwa kumaliza shughuli zote kwa Sh. milioni 56 na mradi umekamilika na unahudumia watu 4,320.

Hata hivyo, amezitaja changamoto kuu zinazoikabili miradi hiyo kuwa ni uharibifu wa vyanzo vya maji unaofanywa na wananchi kwa kuchoma moto ovyo, kulima kwenye vyanzo na kukata miti.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 2, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Mbunge alipoonyesha uliko ufunguo wa kufaulu sayansi**


Ukurasa 12

Utaalamu ETV unavyoongeza matumaini tiba kichwa kikubwa


Ukurasa 13

Pongezi ujio wa vitabu, kazi ni kujenga hamasa kusoma

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU, DODOMA**

# 'Laiti' serikali ingetumia utafiti, ripoti isingepoteza trilioni 1.2/- kila mwaka

KAMA serikali ingechunguza na kufahamu mbinu, na kama ingetumia ripoti za utafiti na taarifa za wataalamu za kitafiti na kutumia mbinu na mikakati ya kuziba mianya ya ukwepaji kodi unaofanywa na kampuni za kimataifa kwenye sekta ya uziduaji hasa madini, Tanzania isingebaki hivi ilivyo leo.

Ni kilio cha vyama shiriki vya shirikisho la asasi zinazotoa huduma kwa umma duniani (PSI) pamoja na asasi za kiraia (AZAKI) nchini zikiiomba serikali kutumia ripoti hizo kukomesha ukwepaji kodi kwenye sekta ya uziduaji (kuchimba madini, mafuta na gesi), hasa eneo la madini unaoliumiza taifa.

Wakizungumza jijini Dodoma kwenye jukwaa lililowakutanisha wadau hao wanasema wakati umefika, serikali ihakikishe Watanzania wanapata elimu ya kujua rasilimali hizo, kuiona mikataba ya uwekezaji wake, wanapata taarifa za mienendo ya kampuni hizo zinazochimba madini na zaidi kuhakikisha kuna uwazi kwenye uwekezaji kwenye uziduaji.

Wanaasasi za kiraia na wataalamu wanasema laiti kampuni za madini zingelipa kodi stahiki na kwa wakati, serikali ingepata fedha nyingi za kugharamia huduma muhimu za jamii kama vile elimu, afya na miundombinu ya barabara mijini na vijijini.

Kadhalika mapato hayo yangeinua sekta nyingine kama kilimo na kuzalisha ajira nyingi, wanasema washiriki wa mkutano huo unaoandaliwa na Shirika la Friedrich Ebert Stftung (FES) la Ujerumani kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama Vinavyotoa Huduma kwa Umma Duniani (PSI).

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa FES Elisabeth Bolrich, anasema idadi ya watu inaongezeka, ni vyema sekta ya uziduaji itumike vyema kupata fedha za kusaidia huduma za jamii mfano elimu, afya na miundombinu kuwafikia raia wanaoongezeka.

Meneja uchambuzi wa bajeti na sera kutoka Shirika lisilo la kiserikali la Policy Forum, Nicholas Lekule, anamuunga mkono akisema wakati umefika serikali kuhakikisha kila mtu na kila kampuni inayofanya shughuli zake nchini inalipa kodi stahiki.

Anasema mapato kutoka sekta ya madini ni muhimu kwa ajili ya huduma za jamii na miradi mikubwa kama miundombinu ya barabara na mradi wa kufua umeme wa bwawa la Mwalimu Nyerere.

"Ukiangalia bajeti ya nchi miradi mikubwa ya maendeleo inategemea wafadhili wa nje na mikopo. Lakini kama kila kampuni ya madini ingelipa kodi stahiki, miradi mingi ya maendeleo na huduma za jamii kama afya, elimu na barabara, ingejengwa kwa kiwango cha juu na mapato yatokanayo na kodi." Anasema Lekule.

Utafiti unaofanywa na Shirika la Action Tanzania mwaka 2020/21 Tanzania inapoteza Dola milioni 531 takribani Shilingi trilioni 1.2 kila mwaka kutokana na misamaha ya kodi kwenye sekta ya uziduaji, anasema Dk. Balozi Morwa.

Dokta Morwa, Mshauri wa Kodi wa shirika hilo, anasema lengo la kampuni yoyote ni kupata aida. Kwa hiyo kampuni zina mbinu mpya, ujuzi, teknolojia na utalaam sana na wakati mwingine kushinda watalaam wazawa.


Waziri wa Madini, Doto Biteko. **PICHA: MTANDAO**

Anasema serikali isipokuwa makini ni lazima ipate hasara kutokana na utalaam wao wa kukwepa kodi.

"Wakati ufike mikataba yao iwekwe wazi, ipitiwe upya na ifuatiliwe kwa kina nje na ndani ya nchi ili kuziba mianya yote ya uwepaji kodi."

Anaungwa mkono na mbunge Cecilia Pareso (viti maalum Arusha), anasema kutokana na utafiti na taarifa za watafiti, nchi



inapoteza kiasi kikubwa mno cha fedha kutokana na makampuni kukwepa kodi na misamaha ya kodi.

"Wito wangu kwa serikali ni utashi wa kisiasa, watumie hizi tafiti za wataalam vizuri kuziba mianya ya ukwepaji kodi unaofanywa na kampuni mbalimbali," anashauri.

Pareso ambaye ni makamu mwenyekiti wa mtandao wa wabunge wa Afrika wapambanaji wa rushwa anasema Tanzania ina sera na sheria za madini nzuri, lakini tatizo ni kwenye utekelezaji na kuishauri serikali itekeleze sera na sheria zilizopo.

Mbunge Constantine Kanyasu wa Geita Mjini, anatoa wito kwa Watanzania kuwa makini katika kusaini mikataba ya madini na kuwataka waungane kufichua wakwepa kodi na rushwa kwa ujumla.

"Kila mtu, Bunge na taasisi mbalimbali zina kazi ya kufanya kutimiza wajibu, tukifanya hivyo tutakuwa tumesaidia serikali kukusanya mapato kwa wingi," anasema.

Mratibu wa Haki Kodi (Tax Justice Project), Daniel Oberko, wa PSI anasema kuwa utekelezaji wa sera na sheria ni lazima ili kukabiliana na ukwepaji kodi kunahitajika utashi wa kisiasa.

Anakumbusha kuwa hilo linawezekana pale kutakapokuwa na mifumo thabiti ya serikali inayofanya kazi kwa uwazi na ushirikiano wa karibu na wadau wote.

"Serikali lazima iamue kuwa inakwenda kutumia mapato kujenga nchi na miradi ya maendeleo ikiwamo huduma za jamii kama elimu, afya na barabara na kuendeleza sekta nyingine kama kilimo na kutengeneza ajira.

Amezitaka AZAKI, vyama shiriki vya PSI na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) na vyama vya wafanyakazi kama TUGHE,

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA

**NA SABATO KASIKA**

# Utaalamu ETV unavyoongeza matumaini tiba kichwa kikubwa

KWA miongo kadhaa, utaalamu uliokuwa unatumika kuwatibu watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa unaosababishwa na maji kujaa kichwani, unafanyiwa upasuaji na kuwawekea mpira (shafti) unaonyonya maji kwenye mishipa iliyoko kichwani na kuyaelekeza tumboni ili yaingizwe kwenye mzunguko wa kawaida.

Lakini, kadri miaka inavyokwenda, ndivyo teknolojia zinaendelea kuvumbuliwa na sasa wataalamu wamekuja na nyingine ambayo inaweza kuwa mbadala wa mpira, inayoitwa Endoscopic Third Ventriculostomy (ETV).

Inaelezwa kuwa ETV ni kifaa ambacho mtoto mwenye kichwa kikubwa anawekewa kichwani, ili kuua sehemu inayozalisha maji, kuzibua mrija ili upitishe maji kwenda katika maeneo (vyumba vinne) vya kichwa.

Vyumba hivyo ni vya kupitisha maji ambayo hayatembei, yanayosababisha kichwa kuwa kikubwa, na kwamba hatua hiyo inayarejesha maji kwenye mzunguko wa kawaida ubongoni.

Daktari Bingwa wa Mishipa na Fahamu, katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), Dk.Hamis Shaban, anabainisha hayo katika kongamano la kujadili vikwazo vinavyowakabili watoto wenye ulemavu huo akieleza kuwa hatua hiyo ni ya kuboresha matibabu.

"Mpira unaweza kuziba kutokana na chembechembe zilizoko katika maji yanayotoka kichwani, kuachana kwenye maungio au kupwaya kichwani na kuleta michubuko," anasema Dk. Shaban.

Anafafanua kuwa katika mazingira hayo, mtoto anaweza kufanyiwa upasuaji zaidi ya mara mbili, lakini ETV imeondoa tatizo hilo, akishawekewa hawezi kufanyiwa upasuaji tena bali maji yatarejea kwenye mzunguko wake.



Janeth akichangia neno katika kongamano. Kulia ni Daktari Bingwa wa Fahamu na Ubongo kutoka MOI, Dk. Hamis Shaban, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Mgongo Wazi (ASBAHT), Abdul-hakim Bayakub na Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dar es Salaam, Judih Kimaro. **PICHA: SABATO KASIKA**

> Tunafadhili mafunzo hayo ambayo hufanyika nchini Uganda na sasa kuna daktari Gerald Mayaya kutoka Hospitali ya Bugando Mwanza ambaye anaendelea na masomo yake.

"Siyo kwamba, uwekaji wa mipira umeachwa, bado tunaendelea nao pale MOI, ni uamuzi wa mzazi au mlezi kuona ni atumie njia ipi kuondoa tatizo hili lakini ninapendekeza ETV," anasema.

### KUINGIA VET TEKNOLOJIA

Janeth Manoni ni Mratibu wa Shirika la Child Help International Kanda ya Afrika lililotoa mafunzo ya teknolojia hiyo kwa baadhi ya madaktari wa Tanzania, anasema Dk. Shaban ni miongoni mwa waliofunzwa naye amekuwa mwalimu wa wenzake wa MOI anaoshirikiana nao kufanya upasuaji huo kwa teknolojia ya ETV.

"Tunafadhili mafunzo hayo ambayo hufanyika nchini Uganda na sasa kuna daktari Gerald Mayaya kutoka Hospitali ya Bugando Mwanza ambaye anaendelea na masomo yake," anasema Janeth.

Anafafanua kuwa akihitimu mafunzo hayo, atarudi na kufundisha wenzake wa Bugando, ili wajue utaalamu huo na kuutumia kusaidia watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa wanaofikishwa katika hospitali hiyo.

"Mafunzo ni ya mwezi mmoja, na gharama yake ni Sh. milioni 25 ambazo Child Help International inalipa na kisha kumpa daktari kifaa cha upasuaji chenye thamani ya zaidi Sh. milioni 100," anasema.

Anafafanua kuwa shirika hilo limeweka milango wazi kwa hospitali ambazo zinataka madaktari wake wakajifunze tekonolojia hiyo ili wawe wanatoa huduma ya upasuaji katika hospitali wanazotoka.

Janeth anasema, shirika hilo lilianza mwaka 2014 nchini Ubelgiji na limekuwa likitoa vifaa tiba mbalimbali na kwamba mwaka 2020 limetoa mipira 1,625 yenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 100.

Anataja baadhi ya hospitali zilizofaidika na msada huo kuwa ni MOI, Bugando, Mnazi Mmoja Zanzibar, Hydom Manyara, lakini pia kujenga nyumba maalum kwa ajili ya wazazi na walezi wa watoto walemavu wanaofika hospitalini kutafuta huduma akiongeza kuwa Mwanza zipo mbili wakati mkoa wa Pwani eneo la Mwandege iko moja na Zanzibar kuna moja.

Katika ufafanuzi wake anasema, uchunguzi wa afya kwa watoto wenye ulemavu huo huchukua muda mrefu na kwamba inabidi wawe na sehemu ya kuishi kwa muda, hasa wale wanaotoka mbali.

### 500 WAHUDUMIWA

Hidaya Alawi ni Mratibu wa Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi (ASBAHT), anasema, tangu teknolojia hiyo kuanza kutumika 2019 watoto zaidi ya 500 wameshafanyiwa upasuaji.

"ASBAHT inaratibu huduma zote za afya kwa wanachama wake, ndiyo maana tunapata takwimu hizo kutoka MOI ambako watoto hupelekwa kufanyiwa upasuaji ili kuwekewa mpira au ETV," anasema Hidaya.

Anaongeza kuwa gharama za upasuaji kwa ajili ya kuwekewa mpira au ETV zinalingana, na kwamba daktari ndiye mwenye kuamua ni njia gani itumike baada ya kumpima mtoto.

"Gharama ya upasuaji ili kuweka mpira wa kunyonya maji kutoka kichwani ni Sh. milioni 1.3 kwa mtoto mmoja, na ndivyo ilivyo hata kwenye ETV, hivyo ni suala la uamuzi tu kuwa ni teknolojia gani itumike," anasema.

## 'Laiti' serikali ingetumia utafiti, ripoti isingepoteza tril. 1.2/- kila mwaka

**INATOKA UK.11**

TALGWU, RAAWU, TUICO na TAMICO kuisaidia serikali katika eneo la utawala bora kwenye sekta ya uziduaji.

"Kazi yetu ni kuisaidia serikali ifanye kazi kwa manufaa ya wananchi wake. Jukumu letu ni kuikazania ilete mabadiliko ambayo imekusudia na imedhamiria kufanya. Ukiangalia sera na sheria za madini zilizopo utagundua kuwa ni nzuri. Nadhani shida ipo kwenye utekelezaji, jambo ambalo linahitaji utashi wa kisiasa.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serkali za Mitaa (TLGWU), Rashid Mtima, anaitaka serikali kudhibiti mianya yote ya upotevu wa mapato ili kupata fedha kusaidia huduma za jamii vijijini.

Kamala Dickson na Peter Ogilo kutoka Shirika la Agenda Participation Initiative (API) wanaeleza umuhimu wa kutekeleza sera na sheria na kuongeza kuwa nchi zinazoendelea zimekuwa zikiendesha miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za wafadhili wakati kuna vyanzo vingi vya mapato ambavyo vingeweza kusaidia miradi hiyo.

Wameishauri serikali kuangalia upya utekelezaji wa sera na sheria na kubana mianya ya wakwepa kodi kupata vyanzo vya fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mkutano huo wa siku mbili uliwakutanisha watalaam kutoka taasisi na vyuo vikuu, masuala ya kodi, watafiti, vyama vya wafanyakazi, wabunge na viongozi wa serikali.

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Pongezi ujio wa vitabu, sasa kazi ni kujenga hamasa kusoma



Kusoma vitabu uwe utamaduni kwa watoto wadogo na watu wazima ndiyo mwanzo wa maarifa. **PICHA: MTANDAO**

WANAFUNZI na walimu shuleni na vyuoni hutumia vitabu kwenye ujifunzaji na ufundishaji. Baada ya mwalimu kumaliza kufundisha darasani kwa kutumia vitabu, mwanafunzi anao wajibu wa kuendelea kusoma vitabu ili kukazia maarifa kwa kile alichojifunza na kupanua uelewa wake katika masuala mbalimbali.

Kuna utajiri mkubwa wa maarifa katika kusoma vitabu ndiyo maana raia katika nchi zilizoendelea wana mwamko mkubwa wa kusoma na kuelewa mambo mbalimbali kutokana na kujisomea.

Ni katika kusoma vitabu huko ndipo wasomaji hujikuta wakiongeza uelewa wa yale wanayoyafahamu na kupata maarifa mapya kila wakati, kufanya utafiti, kuwa wagunduzi na wabunifu zaidi.

Kuyatumia maarifa baada ya kusoma vitabu ndiko kunakoleta matokeo chanya ikiwamo kuibua na kuongeza ubunifu na ugunduzi.

Uwepo wa wanafunzi wengi katika shule za msingi na sekondari kumezalisha tatizo la uhaba wa vitabu. Hali hii inapelekea wengine wengi kuchangia kitabu kimoja, jambo linalodumaza ufanisi kwa wanafunzi kusoma vitabu kwa uhuru na kupata maarifa yaliyomo kwenye vitabuni.

Kutokana na uwepo wa tatizo la uhaba wa vitabu vinavyotosheleza mahitaji, serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka ili kununua vitabu vipya, hatimaye kupunguza tatizo la uhaba huo ambao unawaathiri wanafunzi.

Oktoba 15, 2021, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya elimu, ilizindua utaratibu wa kusambaza vitabu takribani 20,943,989 kuanzia ngazi ya awali, msingi, maandishi yaliyokuzwa pamoja na sekondari vinavyogharimu Sh. bilioni 46.476.

Vitabu hivyo vinavyosambazwa katika halmashauri 184 nchini kwa uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi wawili, ni vya michepuo ya Kiswahili na Kiingreza kwa masomo yote.

Uwekezaji uliofanywa na serikali katika sekta ya elimu hasa kuwajengea uwezo raslimali watu waliomo katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) na taasisi nyingine za elimu ya juu, umewezesha kuwatumia wataalamu kutoka katika maeneo hayo ya elimu kuandaa vitabu hivyo.

> Vilevile, vipo vitabu kwa shule za sekondari vya masomo ya Kemia, Jiografia, Kiingereza, Fizikia, Uraia, Maarifa ya nyumbani (home economics), Baiolojia, Hisabati, Kilimo, Historia na Kiswahili.

Katika uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania, Dk. Aneth Komba, anasema vitabu hivyo viko katika makundi mbalimbali, ambayo ni pamoja na vitabu vya kiada kwa masomo yote ya madarasa ya awali, la kwanza hadi la nne kwa shule zinazotumia Kiswahili na Kiingereza kufundishia.

Aidha, anasema vipo vitabu vya viongozi vya mwalimu I-VII, mihtasari, viongozi vya mwalimu na vitabu vya wanafunzi walio nje ya mfumo rasmi, vitabu vya kundi rika la kwanza mwaka wa kwanza na wa pili na vitabu vya kiada vya kidato cha I hadi IV.

Vilevile, vipo vitabu kwa shule za sekondari vya masomo ya Kemia, Jiografia, Kiingereza, Fizikia, Uraia, Maarifa ya nyumbani (home economics), Baiolojia, Hisabati, Kilimo, Historia na Kiswahili.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, anasisitiza vitabu hivyo vifike shuleni ili wanafunzi wavitumie na kuondoa tatizo la kushindwa kusoma na kuandika.

"Hatutaki kuona mtoto anaingia darasa la tatu hajui kusoma wala kuandika," anasisitiza Ndalichako.

Vitabu ni nyenzo muhimu kwa wanafunzi na walimu katika kufanikisha kazi ya ujifunzaji na ufundishaji, hivyo usambazaji wa vitabu hivi ufanyike na ukamilike ili virahisishe kazi ya walimu na ya wanafunzi na kufanya madhumuni ya wanafunzi kwenda shule kupata maarifa na stadi mbalimbali kufanikiwa kutokana na uwepo wa vitabu vya kutosha kwa uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi wawili.

Wingi wa vitabu hivyo, unatoa nafasi kwa wanafunzi kusoma kwa nafasi bila kugombania kitabu. Ni imani ya Watanzania kuwa vimesheheni maarifa, kwa hiyo kupitia usomaji wa vitabu hivyo, wanafunzi watapata ujuzi na uelewa wa masuala muhimu na ya kutosha yatakayowasaidia na kuwafanikisha kitaaluma na kupata uelewa wa masuala mbalimbali kwa mustakabali wa maisha yao ya sasa na ya baadaye kwenye maendeleo ya taifa.

Wazazi, walezi na walimu wanategemewa kuwajengea wanafunzi utamaduni wa kusoma vitabu ili vitabu hivyo vitakavyofika mashuleni visibaki kuwekwa stoo na maktaba , bali wanafunzi wapewe kwa ajili ya kuvitumia kujisomea na kuelewa masuala muhimu.

Wazazi na walezi wawajengee hamasa watoto wao kuanzia shule za msingi kupenda kusoma vitabu kutokana na utajiri wa maarifa uliopo kwenye vitabu.

Badala ya watoto kusoma majarida mengine yasiyo na tija katika kusoma kwao, wajikite kujifunza kwenye vitabu vilivyopo shuleni na wapunguze muda wa kuangalia runinga majumbani, ili muda mwingi wautumie katika kujisomea vitabu.

Walimu kwa nafasi zao, wasiache kuwahimiza wanafunzi kuazima vitabu ili wajisomee wawapo darasani na nyumbani pia. Walimu wafahamu kuwa kama wanafunzi wao watakuwa na bidii ya kusoma vitabu, hali hii itawarahisishia walimu kazi ya ufundishaji kwani wanafunzi watakuwa na uelewa wa mambo mbalimbali kabla walimu wao hawajafundisha darasani.

Pia utunzaji na uhifadhi wa vitabu hivi uzingatiwe ili viweze kutumika kwa miaka mingi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Kongwa Dodoma.***
***Maoni: 0620-800462.***

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mbunge alipoonyesha uliko ufunguo wa kufaulu sayansi

UNAPOFIKA wakati wa kuchagua tahsusi (combination) ili ziwawezeshe wanafunzi kuendelea na masomo ya ngazi za juu wakifika kidato cha sita na kuingia vyuo vya elimu ya juu, wengi hukimbilia masomo ya sanaa kwakuhofu kuwa sayansi ni ngumu.

Masomo ya sayansi ni pamoja na hisabati, kemia, fizikia, bailojia wakati sanaa inahusisha lugha kikiwamo Kiswahili, Kiingereza na historia. Wanafunzi wanaelezwa kuogopa sayansi kutokana na msingi wake kuwa na hisabati na wengi hawako vizuri kwenye eneo hilo.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, ambaye ni mbunge wa Shinyanga Mjini, ameliona hilo na kuzuru shule kadhaa jimboni kwake, kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi.

Katambi pamoja na hamasa anatoa vitabu vya sayansi, kwa shule nne za sekondari Manispaa ya Shinyanga, pamoja na kompyuta tano na printa katika Sekondari ya Ngokolo, ili kuhamasisha kwa vitendo wanafunzi wasome masomo hayo ambayo ndiyo yanayozalisha wataalamu kuanzia wahandisi, matabibu mpaka manahodha wa meli na rubani wa ndege.

Anasema ili wanafunzi wapende masomo ya sayansi, ni lazima kuwapo na zana za kutosha za kuwafundishia, sababu yanahitaji vitabu na vitendea kazi na ujuzi wa kutosha ndiyo maana ameamua kuanza kutoa vitabu kwanza ili kuwajengea mazingira rafiki ya kusoma.

"Nimegawa vitabu vya sayansi na kompyuta katika sekondari za Manispaa ya Shinyanga, lengo langu ni kuhamasisha kwa vitendo wanafunzi wapende kusoma sayansi, ili nchi yetu ipate wataalamu wake yenyewe na kujiletea maendeleo kwa sababu sayansi ndilo chimbuko la wataalamu,"anasema Katambi.

"Nimetoa vitabu 324 vya masomo hayo na mwongozi wa walimu katika sekondari nne za Chamaguha, Old Shinyanga, Mwamalili na Ibadakuli, ambapo kwa kila moja nimewapa vitabu 81 na kazi hii itakuwa endelevu ili nikamilishe shule zote za jimbo langu," anaongeza Katambi.

Naibu Waziri anasema katika Sekondari ya Ngokolo amewapatia kompyuta tano pamoja




Naibu Waziri Petrobas Katambi (aliyeshika kitabu cha Physics), akiwa kwenye kampeni za kuhamasisha wanafunzi wa shule za sekondari za Shinyanga kupenda masomo ya sayansi. **PICHA: MARCO MADUHU**

> "Nawasihi wanafunzi wa Sekondari za Manispaa ya Shinyanga msome kwa bidii na kupata ufaulu mzuri kwenye mitihani inayokuja, ili msimwangushe Katambi ambaye amewapatia vitabu.

na printa kwa sababu wanatoa elimu ya Teknoloji ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), na kueleza kuwa lengo ni kuwajengea mazingira rafiki wanafunzi kusoma na kutimiza ndoto zao.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Chamaguha iliyoko Manispaa ya Shinyanga, Mwesa Martin, anasema upatikanaji wa vitabu hivyo 81 vya sayansi, utawasaidia kwa kiasi kikubwa kufundisha kikamilifu wanafunzi wa masomo hayo na ni mwanzo wa kufanya vizuri kwenye mitihani yao.

Anasema masomo ya sayansi yanahitaji umakini katika ufundishaji na ujifunzaji, hivyo kukiwapo na upungufu wa vitabu, litatokea tatizo kubwa hasa walimu kufundisha na kumwelewesha mwanafunzi, na ndiyo maana masomo hayo huonekana magumu sababu hayahitaji ubabaishaji wala kutoka nje ya maelekezo.

"Namshukuru mbunge wetu Katambi kutupatia vitabu vya masomo ya sayansi shuleni hapa, ambayo vitaongeza chachu ya wanafunzi kupenda masomo haya pamoja na sisi walimu kutuongezea juhudi ya kufundisha sababu zana za kazi tunazo," anasema Martin.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Ngokolo, Malale Sawaka, anaiomba serikali kuwatatulia pia changamoto ya upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi kwenye shule za sekondari ikiwamo ya Ngokolo, ili kutakapokuwa na vitabu vya kutosha na walimu nao wawepo jambo ambalo litayapaisha masomo hayo pande zote.

Anasema shule hiyo ina wanafunzi 1,240, walimu wapo 37, wanaofundisha masomo ya sayansi ni wanane wakati mahitaji ni 12, na kufanya kuwapo na upungufu wa walimu wanne.

"Tunaiomba serikali ituletee walimu wa kutosha wa masomo ya haya shule kwetu na nyingine, kwani ukienda lazima ukumbane na upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi, hii ni moja ya sababu wanafunzi wengi kushindwa kufanya vizuri kwenye mitihani yao,"anasema Sawaka.

Naibu Meya wa Manispaa ya Shinyanga Ester Makune, anaahidi kuwa serikali itaendelea kushirikiana na Katambi, katika kuzitatua changamoto mbalimbali shuleni ili kuwajengea mazingira rafiki wanafunzi ya kujifunzia na kutimiza malengo yao.

Anawataka pia walimu licha ya changamoto zilizopo shuleni, waendelee kufundisha wanafunzi kwa juhudi zote na kutumia mbinu mbalimbali, wakati serikali ikiendelea na utatuzi wa changamoto za elimu.

"Sisi serikali Manispaa ya Shinyanga, tupo bega kwa bega na Katambi kwa kuhakikisha tunasaidia na utatuzi huu wa masuala ya elimu, na mshukuru pia kwa kutoa vitabu pamoja na kompyuta ili watoto wetu wapende masomo haya na kupata wataalamu wetu," anasema Makune.

"Nawasihi wanafunzi wa Sekondari za Manispaa ya Shinyanga msome kwa bidii na kupata ufaulu mzuri kwenye mitihani inayokuja, ili msimwangushe Katambi ambaye amewapatia vitabu," anaongeza.

Patrician Steven ni mwanafunzi ambaye anasoma katika Sekondari ya Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga, anayesoma sayansi, anasema upatikanaji wa vitabu vya masomo hayo, ni msaada mkubwa kwao kupata uelewa zaidi na hata kufanya vizuri kwenye mitihani yao.

Anasema anapenda sana kusoma sayansi na amekuwa akijitahidi kufanya vizuri kwenye mitihani yake ya majaribio, na kuiomba serikali iendelee kuwawekea mazingira rafiki ya kusoma masomo hayo, pamoja na kuwapatia walimu wa kutosha, ili kusiwepo na changamoto zinazowakwamisha.



## Shule za Fountain zaendelea kutoa matokeo mazuri

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHULE za Fountain Gate Academy zimeendelea kufanya vizuri na kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka huu zimezipita baadhi ya shule kongwe nchini kiwilaya, mkoa na kitaifa.

Kwenye matokeo hayo yaliyotangazwa na NECTA mwishoni mwa wiki, Shule ya Fountain Gate Dodoma imekuwa ya kwanza kati ya 552 za mkoa huo, ya kwanza pia kwenye halmashauri yake kati ya 104 na ya 171 kitaifa kati ya 11,909.

Kwenye matokeo hayo kwa upande wa Fountain Gate Tabata imefanikiwa kuwa ya nne kati ya shule 92 za Wilaya ya Ilala na imekuwa ya 25 kati ya 498 Mkoa wa Dar es Salaam wakati kitaifa imekuwa ya 111 kati ya 11,909.

Mkurugenzi wa shule hizo, Japhet Makau alisema kwa upande wa shule hiyo Tabata wanafunzi 141 ndiyo walifanya mtihani huo na kati yao, 114 wamepata wastani wa alama A na 27 wamepata wastani wa alama B na hakuna C wala D.

Makau alisema hayo ni mafanikio makubwa kwa shule yake kutokana na kuzipita shule kongwe ambazo zilikuwa zikishika nafasi ya kwanza na aliwapongeza walimu wanavyojituma kufundisha mpaka kupatikana kwa matokeo mazuri kama hayo.

Makau alisema haikuwa kazi rahisi kupata matokeo mazuri kiasi cha kuzipita shule kongwe na hivyo walimu wa shule hizo wanastahili pongezi kwani wamekuwa wakifanyakazi usiku na mchana kuhakikisha wanafunzi hao wanaandaliwa vizuri kwa ajili ya mitihani ya kitaifa.

"Nawashukuru wazazi kwa kuendelea kutuamini na kutupa watoto wao tuwalee na kwa mafanikio haya napenda kuwaahidi kwamba hatutabweteka tutaendelea kufundisha kwa bidii kuhakikisha shule zetu zinaendelea kuwa juu kitaaluma na hata siku moja kushika nafasi ya kwanza kitaifa," alisema Makau.

# Wastaafu KAR waomba kumwona Rais Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKARI wastaafu walipigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia (KAR) mwaka 1939 hadi 1945 chini ya ukoloni wa Mwingereza, wameomba kuonana na Rais Samia Suluhu Hassan ili waeleze kero zinazowakabili ikiwamo malipo waliyoahidiwa na Serikali ya Uingereza.

Ombi hilo walilitoa jana kwenye ufunguzi wa kumbukumbu ya miaka 75 ya tamasha la mashujaa la askari waliopigana kwenye vita hiyo na utoaji wa nishani iliyofanyika jijini Dodoma. Akizungumza kwa niaba ya waastaafu hao, Ramadhani Sadiki, alisema waliahidiwa kupewa malipo kama asante yao kwa kazi waliyoifanya na serikali hiyo.

"Hatujawahi kupata hiyo ahadi hivyo tunaamini kama kuonana na Rais wetu atatufanikishia kupata na itatusaidia kutatua baadhi ya changamoto tulizonazo za kila siku."

"Kuna wenzetu wamekufa kutokana na umri na maradhi, basi sisi ambao bado tupo hai, tunamuomba Rais wetu aingilie kati juu ya malipo hayo ambayo hata hivyo hatuna hakika kama zimeliwa au zipo," alisema Sadiki.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Tanzania Legion Clubs, Charles Lubala, alisema watahakikisha wastaafu hao nia yao ya kuonana na Rais inatekelezeka na wanasikilizwa.

Hata hivyo, alisema kuwa lengo kuwapatia wastaafu hao nishani ni pamoja kuelimisha umma wa Tanzania kuhusu umuhimu wa historia na mchango mkubwa uliofanywa na mashujaa hao.

Pia alisema kutunza kumbukumbu na kuwaenzi kwa kuwa ni muhimu kwa vizazi vijavyo.

Kadhalika, katibu huyo alisema kuwa wastaafu hao wamekuwa wakikwamishwa kufikisha kero zao kwa viongozi wa juu kuhusu kupata stahiki zao.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (wapili kulia), akishirikiana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Dk. Khalidi Salumu Mohamed (watatu kushoto), kuzindua nembo maalumu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika mwaka huu yaliyozinduliwa jana, jijini Dodoma. Kulia ni Waziri wa Utamaduni na Sanaa, Innocent Bashungwa, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji (wapili kushoto). **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ndugu wadaiwa kukataa watoto wanapohitimu darasa 7

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MIONGONI mwa kero zinazokikabili kituo cha kulelea yatima cha Nyumba ya Matumaini jijini Dodoma, ni ndugu kuwakataa watoto baada ya kuhitimu darasa la saba.

Mlezi wa watoto katika kituo hicho, Sista Anita Kasanga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na marafiki wa JKT Oljoro (MAO) walipowatembelea na kutoa zawadi kwa watoto pamoja na kusimamia ujenzi wa uzio wa kituo.

Kasanga alisema ndugu wa watoto hao wamekuwa wakiwatelekeza watoto wanapowapeleka kwenye kituo hicho na hata wanapohitimu elimu ya msingi.

"Wakimaliza shule hawataki kuwapokea watoto ili wawaendeleze na elimu ya juu, na kwa sasa kituo hakina wadhamini tunajiendesha wenyewe," alisema.

Vile vile, alisema kituo kina watoto 67 na inakuwa vigumu kuendelea kuwalea wakishakua wakubwa.

Sista huyo alisema wanafunzi wengi wanakataliwa na ndugu zao na baadaye kurejeshwa katika kituo hicho na wao huwapokea ili wasikumbane na ndoa za utotoni.

"Kwa sasa wafadhili wengi hawaleti misaada kutokana na kushindwa kusafiri kwa sababu ya ugonjwa wa corona na wengine wamezeekea na kushindwa tena kutoa msaada," alisema.

Sista Kasanga aliitaka jamii kuendelea kuwasaidia watoto hao na kushukuru marafiki hao kwa kuwajengea ukuta ambao ulikuwa unawapa kero ya mifugo yao kupotea hususani kuku wanaowafuga hapo kwa ajili ya watoto.

Naye Mwenyekiti wa MAO, Joseph Ringo, aliwaasa masista wa kituo hicho kutojisikia wapweke kwa kuwa jamii ipo na itaendelea kuwasaidia kwa misaada mbalimbali.

"Huu ni mwanzo MAO itaendelea kutoa msaada kwa masista hawa ambao wanalea watoto 67, msijisikie wapweke jamii tupo pamoja nanyi kwa kuwa hawa watoto wana uhitaji mkubwa sana katika nyumba hii," alisema.



# 284 wakamatwa Ruaha kwa ujangili hifadhini

Na Grace Mwakalinga, IRINGA

WATU 284 wanaodaiwa kufanya ujangili kwa mwaka 2019/2020 wamekamatwa kwa kujihusisha na uvamizi wa mipaka na kuanzisha makazi na shughuli nyingine za kibinadamu, uwindaji wa wanyama na uvuvi wa samaki katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Uhifadhi Kitengo cha Utalii na Usalama, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Jackson Laizer, alisema idadi hiyo inatokana na jitihada za askari kupambana na majangili, ili kudhibiti matukio hayo yanayokwamisha jitihada za kulinda rasilimali hiyo adhimu ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa pato la nchi kupitia watalii.

Alisema ujangili wanaoendelea kupambana nao ni uvamizi wa mipaka ya hifadhi, uwindaji wa wanyama kama vile swala, pundamilia na uingizaji wa mifugo na kuchunga ndani ya hifadhi na uvuvi wa samaki.

"Kupitia idara yetu ya ulinzi na usalama hapa Ruaha, askari wanafanya doria ya miguu, ndege, boti na gari kuzunguka maeneo yote ya hifadhi, ili kudhibiti vitendo vya ujangili kwa kushirikiana na kitengo cha ujirani mwema tunatoa elimu kwa wananchi juu ya athari za ujangili katika hifadhi,"alisema Laizer.

Aliongeza kuwa katika mwaka 2020/2021 jumla ya majangili 230 walikamatwa katika hifadhi hiyo na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Laizer alisema vitendo vya ujangili vimechangia kwa kiasi kikubwa wanyama kutotulia sehemu moja kwa madai kuwa watalii watembelea hifadhi wanashindwa kuona wanyama wengi kwa sababu wanakimbia wakihofu kuuawa.

Alisema vitendo vya ujangili licha ya kujenga hofu kwa wanyama, lakini inapunguza idadi ya watalii hivyo aliwaomba wananchi kuachana na vitendo hivyo.

Kwa upande wake, Ofisa Habari wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) Kanda ya Kusini, Jacob Kasiri, alisema eneo hilo limebarikiwa vivutio vya utalii vinavyowaleta wengi.



Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Mradi wa Kukuza na Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) wakiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha mkoani Iringa, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa uimarishaji wa miundombinu na usimamizi wa maliasili eneo la kusini mwa Tanzania mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## DC ataka wanahabari kutangaza utalii wa Mbeya

Na Mwandishi wetu, MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, amewaalika wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali Tanzania kwenda mkoani humo kuwekeza kutokana na kuwapo kwa fursa nyingi za kiuchumi.

Dk. Chuachua alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari wanawake kutoka mikoa mbalimbali nchini, ambao walifanya ziara mkoani Mbeya kutangaza vivutio vya utalii na uwekezaji.

Alisema Mkoa wa Mbeya umebarikiwa kuwa na maeneo mazuri ya uwekezaji yenye kuvutia pamoja na miundombinu rafiki ambayo inafaa.

Kutokana na hayo, Dk. Chuachua aliwaomba wanahabari hao kusaidia kuutangaza pamoja na fursa zilizopo ili kukuza uchumi za mkoa na mtu mmoja mmoja kupitia uwekezaji unaofanywa na kuzalisha ajira.

Baadhi ya wanahabari akiwamo, Diana Deus kutoka mkoani Kagera alisema Mkoa wa Mbeya umebarikiwa kuwa na mandhari nzuri ya uwekezaji na mazao ambayo yanachakatwa na kuuzwa maeneo mbalimbali.

Aliongeza kuwa uwepo wa madini wilayani Chunya kumechangia idadi kubwa ya watu kujiajiri na kuajiriwa sambamba na kuongeza pato na halmashauri.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shule za Paradise Pre and Primary School, Ndele Mwaselela, aliwahidi wanahabari hao kuwaunga mkono katika kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii na uwekezaji nchini ili kufungua fursa za ajira na kukuza uchumi wa mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

# 713 waunganishiwa mita za malipo ya kabla

Na Mwandishi wetu, MBEYA

JUMLA ya wateja 713 wameunganishiwa huduma ya mita za malipo ya kabla (Lumaku) kupitia huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya, ikiwa ni mpango mkakati wa kufunga huduma hiyo kwa kila mteja.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya, Gilbert Kayange, akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni alisema mita hizo zilianza mwaka 2015 kwa kuwafungia wateja 50 kama majaribio ya ufanisi na baada ya kubaini utumiaji wake kuwa mzuri waliongeza nyingine na kuzifunga.

Alisema kuwa licha ya mita hizo kuwa na gharama yake kuwa kubwa ukilinganisha na mita za malipo ya baada na kwamba mamlaka imeanza kufanya mita hizo kimkakati kwa kuwafungia wateja wa taasisi, biashara na baadhi ya wateja wa majumbani.

"Katika kuboresha huduma hiyo na kuhakikisha inawafikia wananchi mamlaka hiyo katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kununua mita za Lumaku 1,000 na kwamba zitawafikiwa wateja wote," alisema Kayange.

Kuhusu wimbi la vishoka mitaani, Kayange alisema ni miongoni mwa vikwazo vinavyoikabili mamlaka hiyo kwa sababu wanachangia kwa kiasi kikubwa maunganisho ya maji yasiyokuwa halali kitendo ambacho kinainyima serikali mapato huku wengine wakikosa huduma ya maji kikamilifu.

Alisema mamlaka hiyo inashirikiana na wadau mbalimbali vikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa serikali wa eneo husika na wasamaria wema kupata taarifa za wizi wa maji.

Aliongeza kuwa mwaka 2020/2021 jumla wa watuhumiwa 23 walikamatwa kwa kosa la kuwaunganishia wateja huduma ya maji kinyemela na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria na kwamba wanaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali huku wakitoa dau la Sh. 200,000 kwa yeyote atakayefanikisha kutoa taarifa za uwepo wa vishoka.

Kayange aliwahakikishia wakazi wa Mbeya kuendelea kupata huduma ya majisafi na salama kwa wakati bila upendeleo na kutoa taarifa pindi linapojitokeza tatizo.

Hivi karibuni baadhi ya wananchi walitoa malalamiko juu ya mamlaka hiyo kwamba inatoa huduma za maji kwa upendeleo ukiwamo utaratibu wa kujiunga na huduma hiyo kwamba wanatoa kipaumbele kwa mtu wanayemfahamu.

Kayange alisema mamlaka hiyo inafuata utaratibu kwa wateja wale ambao wamekamilisha mahitaji yote ya maunganisho ya huduma mapema na kuhusu mgao, alisema unajulikana kwa maeneo yanayopata maji kwa mgao kama Uyole, Isyesye, Ituha, Shewa na baadhi ya maeneo ya Sae.



# Chanjo Uviko-19 sasa yapokelewa kwa hamasa

**Na Rahma Suleiman**,
ZANZIBAR

MRATIBU wa Huduma ya Elimu ya Afya Zanzibar, Halima Ali Khamis, amesema mitazamo hasi dhidi ya chanjo ya corona Zanzibar mwanzoni hayakuwa mazuri ikilinganishwa na sasa.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe baada ya kumalizika kwa mafunzo ya uhamasishaji wa chanjo ya corona kwa waandishi wa habari yaliofanyika Kariakoo, mjini hapa.

Alisema takribani watu 50,000 wameshachanja chanjo ya corona na kundi la wazee linaongoza zaidi ikilinganishwa na makundi mengine.

"Wazee kutokana na hatari walionayo wamejitokeza kwa wingi kupata chanjo ikilinganishwa na makundi mengine kama ya vijana," alisema.

Alisema kati ya watu 50,000 waliopata chanjo wanaume wanaongoza ikilinganishwa na wanawake kutokana na chanjo hizo awali kuwa na kasumba mbalimbali hasa kwa wanawake.

Alisema miongoni mwa kasumba hizo ni kuwa chanjo hizo zinazuia kizazi kwa wanawake, kuvimba bega au kupata siku za hedhi kabla ya wakati na mwanamke ni mwenye majukumu mengi ya familia huvunjika moyo kupata chanjo.

Alisema baada ya elimu ya chanjo kuenea hivi sasa wanawake wanajitokeza kupata chanjo hiyo baada ya kugundua kuwa kasumba zilizokuwa zikienezwa Hazina ukweli.

Aliwataka wananchi kuendelea kujitokeza kupata chanjo ili kupunduza kasi ya maambukizi na hali mbaya ya maradhi ya corona.

"Chanjo itatuweka huru kuendelea na kazi zetu...tuitumie fursa hii tuliyoipata chanjo inatolewa bure bila ya malipo hivyo tuitumie fursa hii kabla haijawa kwa malipo," alisema.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo kwa waandishi wa habari, Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema katika wimbi la tatu la ugonjwa wa corona watu 70,000 waliopimwa Zanzibar 1,400 wamekutwa na maambukizi.

Aidha, alisema kuwa utoaji wa huduma za chanjo ni mkakati muhimu wa kuikinga jamii dhidi ya ugonjwa huo, Wizara ya Afya, imejizatiti ili kuhakikisha huduma hizo zinatolewa kwa walengwa wote katika vituo vilivyowekwa vya kutolea chanjo ya Uviko-19.

## Mwinyi kuzungumzia mafanikio mwaka 1 wa uongozi wake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajia kuzungumza na waandishi wa habari Novemba 6, mwaka huu, kuelezea mafaniko ya mwaka mmoja wa uongozi wake katika Serikali ya Zanzibar.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja Idrissa Mustafa Kitwana, alisema kabla ya mkutano huo wa Rais na waandishi wa habari pia kutakuwa na shughuli mbalimbali ikiwamo uzinduzi wa miradi katika kusherehekea mwaka mmoja wa Dk. Mwinyi. Alisema kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja ya uongozi wa Dk. Mwinyi mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwamo kuimarika kwa hali ya usalama na amani ya nchi.

Alisema miongoni mwa mafanikio hayo ni watu kuishi kwa kushirikiana na kuondokana na siasa za chuki na uhasama ambazo zilikuwa zikisababisha mitafaruku katika jamii.

"Mafanikio zaidi ya mwaka mmoja ya uongozi wa Dk. Mwinyi atakuja kuwaeleza Novemba sita mwaka huu nisimalize maneno," alisema Kitwana.

Alisema miradi ambayo itafunguliwa itaakisi dhamira ya dhati ya kupunguza umaskini nchini.

Alisema miradi hiyo itaongeza ajira kwa wananchi kupitia sekta binafsi ikiwa ni ahadi ya Rais wa Zanzibar ya kutoa ajira 300,000 ambazo zitatokana na sekta mbalimbali.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na uzinduzi wa nyumba za kibiashara, kiwanda cha kutengeneza vipodozi katika Mkoa wa Mjini, uwekaji wa mawe ya msingi wa hoteli ya Lagema na Palolo Mkoa wa Kaskazini, hoteli ya Oasisi Mkoa wa Kusini Unguja pamoja na mradi wa kiwanda cha maji ya kunywa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema katika maadhimisho hayo kutakuwa na shughuli za usafi kitaifa zitakazofanyika katika mikoa yote ya Zanzibar.

Kaulimbiu ya mwaka mmoja ya uongozi wa Dk. Mwinyi ni 'Neema ya amani na umoja wetu, safari ya ujenzi wa uchumi mpya, inaendelea'.



Balozi wa Marekani nchini Tanzania Donald Wright (kulia), akiwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhamed Said, akiendesha baiskeli nje ya wizara hiyo, Mazizini Unguja wakati alipomtembelea. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yaeleza umuhimu wa utafiti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Hamad Rajab, amesema uzinduzi wa utafiti wa sheria ya habari utasaidia kufahamika kwa sheria za habari nchini.

Aliyasema hayo jana mjini hapa katika kikao cha uzinduzi wa taarifa ya marekebisho ya Sheria ya Habari ya Zanzibar.

Alisema utafiti huo umekuja muda muafaka wakati Serikali ya Zanzibar inaifanyia kazi Sera na Sheria za Habari ili ziendane na mazingira ya sasa na kutoa fursa kwa tasnia ya habari.

Alisema serikali kupitia wizara yake ni sikivu na imepokea mapendekezo ya wadau kuhusu haja ya kufanyiwa marekebisho au kuwapo kwa sheria mpya ya habari Zanzibar.

"Hakuna anayekataa umuhimu wa sekta hii ya habari kwa nchi yoyote," alisema.

Aliwataka waandishi wa habari kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao na kutumika kujenga umoja, kuimarisha demokrasia, kukuza utawala bora na kuimarisha uchumi.

Alisema ni vyema nguvu ya vyombo vya habari itumike kujenga badala ya kubomoa, kuhamasisha umoja na kujiepusha na kauli za chuki.

Naye mshauri elekezi wa masuala ya sheria, Dk. Chris Maina Peter, alisema waandishi wa habari wanahitaji kuwapo kwa sheria nzuri ambazo zitawasaidia kutekeleza majukumu yao bila ya kuwa na hofu kwa ajili ya kuibua changamoto za wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya waandishi wa habari wa Zanzibar, mwandishi mwandamizi Salim Said Salim, alisema wakati umefika Zanzibar kuwa na sheria ya waandishi wa habari ambayo itatekeleza majukumu yao bila ya kuingiliwa uhuru wao na vyombo vya dola.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

GARI INAUZWA AINA YA VOLKSWAGEN TOUREG YA MWAKA 2004 NAMBA DDV RANGI NYEUSI. INATEMBEA NA IKO KWENYE HALI NZURI SANA. BEI NI TSH. 15,000,000/- PIGA SIMU NAMBA 0762 810 451.

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPH .A. MALICK** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2381-0160** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TURIANI SEKONDARI** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/520378/2021.**

116547402

## PASSPORT IMEPOTEA



HALIFA ABDALLAH MOHAMED anatangaza kupotelewa na PASSPORT No. TAE291024 iliyotelewa 20January,2020 na kuishia 29 January,2030.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/520796/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

MOHAMMED ENTERPRISES (T) LTD anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI aina ya BAJAJ BOXER yenye namba za usajili MC 533 CHV.Chasis No. MD2A21-BY0KWB89334, Engine No. PFZWKB32766. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DOM/DOM/R-B/519766/2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MKOA WA KILIMANJARO**
**MAHAKAMA YA MWANZO BOMANGOMBE**
**WILAYA YA HAI**
**SHAURI LA TALAKA NA. 23/2021**

**MDAI……………………………………………….. ALEX ROBSON MUSHI**
**MDAIWA………………………………………… STELA NICHOLAUS MUSHI**
**KWA :STELA NICHOLAUS MUSHI**

**POPOTE ULIPO TANZANIA BARA NA VISIWANI**
Shauri tajwa hapo juu limefunguliwa katika Mahakama ya mwanzo Bomangombe . Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 4/11/2021 saa 8:30 asubuhi fika bila kukosa usipofika Mahakamani shauri litasikilizwa upande mmoja .

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
BOMANG'OMBE.

## DEEP POLL
**The registration of the Document Act (Cap. 117)**

By this Deed I, the undersigned **IDDI MAJIO IDDI** of P.O. Box 178 Tanga. Do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former names **IDDI MAJIO BWANGABWA** and in lieu thereof do assume from the date hereof the name of **IDDI MAJIO IDDI.** In pursuance of such change of my name, I hereby declare that I shall at all times herein after in all records, deeds and instructions, in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **IDDI MAJIO IDDI** in lieu names of **IDDI MAJIO BWANGABWA** so renounced as aforementioned. **AND** I hereby authorize and request all persons to designate, describe and address me by such assumed name of **IDDI MAJIO IDDI.**
In witness whereof, I have hereunder signed my assumed name of **IDDI MAJIO IDDI** in lieu of the relinquished name **IDDI MAJIO BWANGABWA.**
**SIGNED** and **DELIVERED** by the said **IDDI MAJIO IDDI** who is known/identified to me by

The latter being known to me in my presence
This ..31... day of ........ 2021
Before me........
Signature........
Qualification........
Address........
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

116547902

VANILLA International Ltd

## TAARIFA KWA UMMA

Hivi karibuni kumekuwa na kipeperushi kikisambaa mitandaoni kuhusu Vanilla International Ltd kikitaja majina ya watu na nyadhifa zao kuwa ni wadau/wateja (stakeholders/clients).

Tunakanusha kuwa kipeperushi hicho siyo cha Vanilla International Ltd, bali kimesambazwa kwa lengo ovu la kuichafua Vanilla International Ltd. Kwa taarifa hii, Vanilla International Ltd inakanusha vikali kuwa kipeperushi hicho siyo cha Vanilla International Ltd na hivyo jamii ipuuze taarifa hiyo. Vanilla International Ltd inaomba radhi kwa usumbufu wowote uliotokana kwa jina lake kutumika kwa lengo ovu.

**IMETOLEWA NA MKURUGENZI WA VANILLA INTERNATIONAL LTD**
**SIMU 0629300200**

216548002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROSE .Z. ISSAYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 747 CGS – MITSUBISH CANTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/4866/2021.**

116548202


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mbunge Uingereza afanya harambee kumtunza mtoto

**London,** UINGEREZA

MBUNGE wa Uingereza amewataka watu kushiriki katika mchango wa fedha mtandaoni kwa Mkenya anayedaiwa kuuawa na wanajeshi wa Uingereza ambazo zitasaidia familia ya marehemu ikiwamo malezi ya mwanawe.

Mbunge wa Chama cha Labour, Jess Phillips, alianza harakati za kusaidia familia ya Agnes Wanjiru ambayo ilibidi kumlea binti aliyemuacha baada ya kuuawa.

**Hatuwezi kurekebisha kosa hili lakini tunaweza kuonyesha ubinadamu wetu.**

Phillips alisambaza mtadaoni makala ya Sunday Times kuhusu madai ya machapisho ya Facebook ya askari wa Uingereza akifanya utani kuhusu mauaji hayo.

"Hatuwezi kurekebisha kosa hili lakini tunaweza kuonyesha ubinadamu wetu," alisema kupitia ujumbe wa twitter:

Mchango huo wa crowdfund umevuka paundi 7,000 (sawa na dola 9,500) na malengo ni kuongeza hadi paundi 10,000."

Wanjiru alidaiwa kuuawa na mwanajeshi mmoja wa Uingereza mwaka wa 2012 na mwili wake kupatikana kwenye tangi la choo katika hoteli, miezi mitatu baada ya kuonekana na wanajeshi hao.

Wizara ya Ulinzi ya Uingereza ilisema inashirikiana na uchunguzi wa Kenya kuhusu kifo chake baada ya ripoti ya Sunday Times. **BBC**



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, akimsalimia Rais wa Comoro, Azali Assoumani, alipowasili jijini Glasgow, nchini Scotland kuhudhuriwa mkutano wa mabadiliko ya tabianchi COP26. Mkutano huo unakutanisha viongozi takribani 120 kutoka nchi mbalimbali duniani. **PICHA: BBC**

## Uganda yafungua vyuo baada ya 'lockdown' miezi 5

**Kampala,** UGANDA

VYUO vikuu pamoja na taasisi nyingine za elimu ya juu, vimefunguliwa tena, baada ya kufungwa katika mwanzo wa janga la wimbi la pili la maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 Juni, mwaka huu.

Wanafunzi wapatao 260, 000 wanasoma katika vyuo vikuu na katika taasisi nyingine za elimu ya juu Uganda.

Mwandishi wa BBC mjini Kampala, alisema Chuo kikuu cha zamani na kikubwa zaidi nchini humo cha Makerere, kimefunguliwa tu kwa wanafunzi waliojiunga kwa mwaka wa kwanza mwaka 2019, pamoja na wahitimu.

Tayari masomo yamekwishaanza katika baadhi ya maeneo.

Baadhi ya wanafunzi waliiambia BBC kwamba wanaona hawatoweza kumaliza masomo yao kwa muda waliotarajia, kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kuhudhuria masomo kwa njia ya mtandao wakati vyuo vikuu vilipofungwa.

Vyuo vikuu viliendelea na masomo kwa njia ya mtandao wakati vilipofungwa, baadhi ya wanafunzi, hususan wale wanaoishi katika maeneo ya vijiji vya mbali, walikabiliwa na changamoto ya kupata mawasiliano ya mtandao au hata kukosa uwezo wa kulipia gharama za mtandao.

Vyuo vikuu vyote 282, vyuo vya ufundi na taasisi nyingine za elimu ya juu kote nchini vinakabiliwa na changamoto zinazofanana. **BBC**

## Mwanamume aliyebeba kisu ajeruhi 17

**Tokyo,** JAPAN

MWANAMUME mmoja ametekeleza shambulio la kisu ndani ya treni jijini Tokyo na kisha kuwasha moto kwenye treni hiyo.

Watu 17 wamejeruhiwa akiwamo mzee mwenye umri wa miaka ya 70 aliyedungwa kisu na anaripotiwa kupoteza fahamu.

Aliyetekeleza shambulio hilo amekamatwa.

Polisi walisema wakati akiwa ndani ya treni iliyoelekea kituo cha Shinjuku, mwanamume huyo alianza kuwashambulia abiria karibu na kituo cha Kokuryo katika mji wa Chofu uliopo magharibi mwa Tokyo.

Walisema pia alitumia kiwasha sigara kuwasha moto ndani ya treni.

Moto mkubwa uliwaka kwa muda mfupi na kuchoma baadhi ya viti.

Treni hiyo ilisimama kwa dharura kituoni Kokuryo na kuwaruhusu abiria kukimbilia kwenye jukwaa.

Polisi walimkamata Hattori Kyota kwa tuhuma za kujaribu kutekeleza mauaji. **NHK**

## Vikosi vya waasi wa Tigray na Oromo vyadai kuteka miji Ethiopia

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

MAKUNDI mawili tofauti yanayopambana dhidi ya serikali kuu ya Ethiopia, yanasema yameteka miji siku ya Jumapili, huku Waziri Mkuu Abiy Ahmed akiwatolea wito raia kujiunga na mapambano, katika mzozo unaozidi kushika kasi.

Waasi wa Tigray wametangaza Jumapili kuuteka mji wa kimkakati kaskazini mwa Ethiopia, serikali ilikanusha madai hayo, na kusema vikosi vya shirikisho vilikuwa katika mapigano makali ya kuutetea mji huo wa Kombolcha na mji mwingine wa Dessie.

Iwapo itathibitishwa, kutekwa kwa Kombolcha Jumapii, kunakojiri siku moja baada ya waasi kudai kuudhibiti mji wa Dessie, itakuwa mafanikio ya kimkakati kwa wapiganaji wa Tigray dhidi ya jeshi la Ethiopia na washirika wake, wanaojaribu kuwafurusha Watigray kutoka mkoa wa Amhara.

Msemaji wa Chama cha Ukombozi wa Watu wa Tigray TPLF, Getachew Reda, alisema kupitia ukurasa wa twitter kuwa wapiganaji wake wameiteka Kombolcha na uwanja wake wa ndege. **DW**

## China yafungua tena biashara Afghanistan

**Beijing,** CHINA

CHINA imefufua tena biashara za moja kwa moja kwa njia ya ndege na Afghanistan katika juhudi ya kulisaidia taifa hilo lililoathiriwa na vita vya muda mrefu pamoja na kuwezesha viongozi wapya wa Taliban kukabiliana na matatizo ya kiuchumi na kibinadamu yanayoendelea kushuhudiwa.

Ndege ya mizigo iliyokuwa imebeba tani 45 za mbegu za Pine, Jumapili iliondoka kwenye uwanja wa ndege wa Kabul kuelekea kwenye masoko ya China, ikiashiria ukurasa mpya wa kibiashara kati ya mataifa hayo tangu Taliban kukamata serikali, Agosti.

Msemaji wa Serikali ya Taliban, Bilal Karimi, aliiambia VOA kwamba wanatumai shughuli za kibiashara zitaendelea kuimarika kati ya taifa lake na China. **VOA**

# NJE YA DIMBA NA STARS KUANZA KUPELEKA NYOTA KWA MASHABIKI

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa Timu ya Taifa, Taifa Stars, wametakiwa kukaa mkao wa kuwapokea wachezaji nyota wa timu hiyo ambao watakuwa wakizunguka sehemu mbalimbali nchini kwa udhamini wa Bia ya Serengeti Lager chini ya Kampeni ya Nje ya Dimba na Stars iliyozinduliwa hivi karibuni.

**Kampeni hiyo ambayo itakuwa ya nchi nzima, itadumu kwa miezi mitatu huku ikilenga kuwapa nafasi mashabiki wa Taifa Stars kukutana na nyota wanaowapenda katika baa zao na pia watapata fursa ya kuwauliza maswali kuhusu maisha yao nje ya soka pamoja kupiga nao picha za ukumbusho.**

Kwa mujibu wa Meneja Mwandamizi wa Chapa ya Serengeti Breweries Limited (SBL), Wankyo Marando, Bia ya Serengeti Lager ikiwa kama shabiki mkuu wa Taifa Stars, inajivunia kuwaletea mashabiki wa timu hiyo, nyota wanaowapenda na kuwapa nafasi ya kuzungumza nao ili kuwafahamu kwa undani zaidi.

"Shabiki mkuu na mdhamini wa timu yetu ya Taifa, Taifa Stars, Bia ya Serengeti Lager leo inayo furaha kuzindua Kampeni ya Nje ya Dimba na Stars inayolenga kuwakutanisha mashabiki uso kwa uso na nyota ambao mara nyingi wamekuwa wakiwaona uwanjani. Hii ni fursa pekee ya mashabiki kujua maisha ya nyota wao nje ya uwanja," alisema Wankyo.

Wankyo alisema kampeni hiyo ya nchi nzima itahusisha wachezaji wa Taifa Stars ambapo watatembelea mikoa ya Mbeya, Mwanza na Arusha na kukutana na mashabiki wao kupitia matukio kama pati za mwisho wa mwezi Nje ya Dimba na Stars ambapo kwenye matukio kama hayo mashabiki wataweza pia kujishindia zawadi mbalimbali na ofa za bei yao pendwa ya Serengeti Lager.

"Wachezaji watakuwa kwenye baa mbalimbali na wakati wateja wetu wa Bia ya Serengeti Lager wakiendelea kuburudika na bia yao pendwa iliyotengenezwa kwa kimea kwa asilimia 100 na isiyoongezwa sukari, watapata nafasi ya kuwauliza maswali, kupiga picha na kupata sahihi zao," alisema.

Kwa upande wa Nohodha Msaidizi wa Taifa Stars, Erasto Nyoni, alisema wachezaji wamefurahi kupata fursa ya kukutana na mashabiki wao na kuwataka wajitokeze kwa wingi ili wafahamu maisha ya wachezaji nyota wanaowapenda nje ya uwanja.

"Kwa niaba ya wachezaji wenzangu, napenda kuishukuru Bia ya Serengeti kwa fursa hii ya kutukutanisha na mashabiki wetu. Tunawaahidi mashabiki kuwa tutakuwa tayari kujibu kila swali watakalouliza na tutafurahi kupiga nao picha," alisema Nyoni.

Wankyo aliwataka mashabiki wa Stars kutembelea kurasa za mitandao ya kijamii ya Bia ya Serengeti Lager pamoja na kusikiliza redio kwa ajili ya kujua lini na wapi nyota wa Taifa Stars watakuwa.




Baadhi ya mashabiki wa Timu ya Taifa, Taifa Stars, wakipiga picha (Selfie) na wachezaji nyota wa timu hiyo Kibu Denis (wapili kushoto) na Kennedy Juma, muda mfupi baada ya uzinduzi wa Kampeni ya Nje ya Dimba na Stars inayowapa nafasi mashabiki kukutana na wachezaji nyota wanaowapenda uso kwa uso katika baa zao. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Biashara yamwagiwa mamilioni ya udhamini

**Na Faustine Feliciane**

KLABU ya Biashara United ya Mara, imeingia mkataba wa udhamini na Kampuni ya Uchimbaji wa Madini ya Barrick North Mara, wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 310 kwa kipindi cha msimu mmoja.

Mbali na pesa hizo, pia North Mara itatoa kiasi cha dola 45,000 (zaidi ya Sh. milioni 100) kwa timu hiyo kwa ajili ya michuano ya kimataifa ili kuiwezesha kushiriki kikamilifu.

Akizungumza jana wakati wa kutiliana saini mkataba huo mbele ya Katibu Tawala Mkoa wa Mara, Albert Msovela, Katibu wa klabu hiyo, Haji Mtete, alisema udhamini huo utaondoa baadhi ya changamoto zinazowakabili.

Alisema anaishukuru kampuni hiyo kwa kukubali kusaini tena mkataba mpya ambao utawapa uhakika wachezaji wa timu hiyo kupata stahiki zao na kujituma uwanjani kwa ajili ya timu.

Aidha, Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Apolinary Lyambiko, alisema uimara wa uongozi na kujituma kwa wachezaji kumewafanya kukubali kusaini mkataba huo.

Kwa upande wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Msovela, aliishukuru North Mara na kuwataka wananchi wa mkoa huo kujitokeza kuisapoti timu hiyo ili kuweza kufanya vizuri.

Biashara inaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika ambapo hatima yao ya kusonga mbele bado ipo mikononi mwa CAF baada ya kushindwa kusafiri kwenda kwenye mchezo wa marudiano hatua ya pili dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya baada ya mchezo wa awali Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kushinda mabao 2-0.

# Redondo aitwa Taifa Stars kuivaa DR Congo

**Na Saada Akida**

HATIMAYE kiungo mshambuliaji wa Biashara United, Ramadhan Chombo 'Redondo' amejumuishwa katika kikosi cha wachezaji 27 cha timu ya Taifa, Taifa Stars, kilichotangazwa jana kujiandaa na michezo miwili ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar dhidi ya DR Congo na Madagascar.

Hii ni mara ya kwanza kwa Redondo kuitwa Taifa Stars, lakini aliwahi kuitwa katika timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), wakati ikishiriki michuano ya Chalenji ikiwa chini ya Kocha Boniface Mkwasa.

Wachezaji wengine waliorejeshwa baada ya kukosa mchezo uliopita dhidi ya Benin ni Shomari Kapombe na Erasto Nyoni waliokuwa majeruhi pamoja na Mzamiru Yasin aliyekuwa na adhabu ya kadi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijni Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen, alisema wanaenda kwenye michezo muhimu ya kukamilisha ratiba ya kufuzu Kombe la Dunia, hivyo wanahitaji kushinda.

"Katika kikosi changu nimemwongeza mchezaji mmoja, Redondo, ambaye amekuwa na kiwango kizuri akiwa na Biashara United, ni mchezaji mzuri mwenye uzoefu na michuano tofauti, nimemfahamu kwa muda mrefu," alisema Poulsen.

Alisema anafurahi kwa sababu timu yake inashika nafasi ya kwanza katika kundi lake, lakini ni ndio timu iliyofunga mabao mengi huku pia ikiwa na uwezo mzuri wa kujilinda.

Kocha huyo aliwaomba Watanzania kuendelea kuisapoti timu yao kwani inaingia kucheza michezo muhimu zaidi, hivyo inahitaji kusapotiwa ili iweze kutimiza malengo yake.

Kikosi cha Stars kilichoitwa ni makipa; Aishi Manula, Metacha Mnata na Ramadhan Kabwili huku mabeki wakiwa ni Kibwana Shomari, Shomari Kapombe, Israel Patrick, Edward Charles, Mohamed Hussein, Erasto Nyoni, Dickson Job, Bakari Mwamnyeto, Kennedy Juma , Lusajo Mwaikenda na Nikson Kibabage.

Viungo ni Meshack Mwamita, Novatus Dismas, Mzamiru Yasin, Ramadhan Chombo, Zawadi Mauya na Feisal Salum. Washambuliaji ni John Bocco, Iddi Seleman 'Nado', Abdul Suleiman, Mbwana Samata, Kibu Denis, Reliant Lusajo na Simon Msuva.

Taifa Stars ambayo ni kinara wa Kundi J, itaingia kambini Alhamisi wiki hii kujiandaa na mchezo dhidi ya DR Congo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Novemba 11 kabla ya Novemba 14, mwaka huu kushuka dimbani nchini Madagascar dhidi ya wenyeji wao hao.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POGBA, RUDIGER WAWANIWA**

REAL Madrid wanamwangalia kwa karibu kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, pamoja na mlinzi wa Chelsea na Ujerumani, Antonio Rudiger, 28, kama wachezaji wapya wanaoweza kusaini nao mkataba katika klabu hiyo. ***(Marca)***

**BARCA WAMTAKA DE BEEK**

BARCELONA wanania ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa kati wa Manchester United na Uholanzi, Donny van de Beek, 24. ***(Sport)***

**CONTE KUMRITHI NUNO**

TOTTENHAM inataka kumchukua Antonio Conte kuchukuwa mikoba ya Nuno Espirito Santo kama kocha mpya. ***(Tuttomercato)***

**CONCEICAO AFIKIRIWA**

KOCHA wa Porto, Sergio Conceicao, 46, pia anafikiriwa kuchukuwa nafasi ya Nuno Espirito Santo kama kocha mpya pale Tottenham. ***(Standard)***

**MASON KOCHA WA MUDA**

RYAN Mason, 30, atateuliwa kuwa kocha wa muda wa Tottenham hadi Krismas. ***(Football Insider)***

**PSG YAMWANIA POGBA**

KLABU ya Paris St-Germain inafuatilia kwa karibu hali ya Paul Pogba pale Manchester United. ***(Le10 Sport)***

**HERNANDEZ AIKATAA CITY**

MLINZI wa kushoto wa Ufaransa, Theo Hernandez, 24, anapanga kukataa kuhamia Manchester City ili asaini mkataba mpya pale AC Milan. ***(Calciomercato)***

**UTD WASHINDWA KWA GUEYE**

MANCHESTER United ilishindwa kumsajili kiungo wa PSG na Senegal, Idrissa Gueye, 32, kipindi cha majira ya joto kilichopita, kwa sababu walishindwa kutoa ofa yoyote kutokana na wachezaji wengi kutoondoka. ***(Mail)***

**GOUIRI AWINDWA MAN CITY**

MSHAMBULIAJI wa Nice na Ufaransa, Amine Gouiri, 21, anawaniwa na Manchester City. ***(Fichajes)***

**VLAHOVIC AITAKA REAL**

STRAIKA wa Fiorentina na Serbia, Dusan Vlahovic, 21, anataka kujiunga na Juventus. Mchezaji huyo pia anahusishwa na Manchester City. ***(Tuttosport)***

**WINKS AGOMBEWA EPL**

EVERTON na Aston Villa zinaongoza kwenye mbio za kuwania usajili wa kiungo wa Tottenham na England, Harry Winks, 25, Januari. ***(Caughtoffside)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# IBRAHIMOVIC: NAAMINI AC MILAN ITABEBA TAJI SERIE A

## ●●● Tunaamini katika hili, tumefanya vizuri hadi sasa, lakini msimu bado mrefu na...

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic amesema anaamini AC Milan wapo kwenye nafasi kubwa katika mbio za ubingwa wa Serie A baada ya kuendelea kuwa na mwanzo bora wa msimu huu kwa kuifunga AS Roma, lakini straika huyo amekiri safari bado ni ndefu.

Milan iliifunga Roma 2-1 pale kwenye Uwanja wa Olimpico Jumapili, huku Ibrahimovic akifunga bao la ufunguzi akiwa umbali wa yadi 25 kwa shuti la adhabu ndogo, na kumfanya kufikisha mabao 400 ya ligi katika maisha yake ya soka - 150 kati ya hayo akifunga kwenye Serie A.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 40 raia wa Sweden, alipata penalti iliyozaa bao la pili kwa timu yake, likifungwa na Franck Kessie dakika ya 57, kabla ya Stephan El Shaarawy kufunga la kufutia machozi.

**Ushindi huo maana yake Milan imefikisha pointi 31 kwenye mechi 11 za Serie A, wakiwa nyuma ya vinara Napoli ambao wanaongoza kwa tofauti ya bao moja.**

Milan imekuwa timu ya nne kwenye historia ya Serie A kushinda mechi 10 kati ya 11 za msimu, baada ya Roma, Juventus (mara mbili) na Napoli (mara mbili).

"Tutajaribu. Tunaamini katika hili, tumefanya vizuri hadi sasa, lakini msimu bado ni mrefu na tunatakiwa kuwa kwenye kiwango hiki," alisema Ibrahimovic akiiambia DAZN baada ya mchezo huo kuhusu matarajio yao kwenye mbio za ubingwa. "Tunaamini, lakini ni siku za mwanzo kabisa. Safari bado ni ndefu ingekuwa imebaki mechi moja sawa."

Rossoneri hao kwa mara ya mwisho walitwaa taji la Scudetto msimu wa mwaka 2010-11, na walikabiliwa na wakati mgumu hadi msimu uliopita kumaliza nafasi ya pili.


MECHI KALI
HOME
AWAY
ATALANTA
2.59 | 3.66 | 2.50
MANCHESTER UTD

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS. 642

# MESSI ATANGAZA NIA KURUDI BARCELONA



**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Lionel Messi, anataka kurudi Barcelona baada ya siku zake za kucheza kumalizika kama katibu wa ufundi.

Messi alitumia miongo miwili pale Barcelona, akiwa mfungaji wa wakati wote wa klabu hiyo na pia aliyecheza mechi nyingi zaidi, na akajiunga na PSG kabla ya kuanza kwa msimu huu wa 2021-22.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, aliondoka kwa miamba hao wa LaLiga baada ya timu hiyo kukabiliwa na matatizo ya kifedha yaliyozuia kumpa mkataba mpya nyota huyo wa kimataifa wa Argentina.

Lakini Messi ameelezea nia yake ya kutaka kurudi Barca, ambako alishinda mataji 35 yakiwamo 10 ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ndio, mara zote nimekuwa nasema ningependa kurudi kuisaidia klabu kwa njia yoyote," alisema Messi, ambaye hajaifungia PSG bao kwenye Ligue 1, akiiambia Sport.

"Nataka kutumika na kuisaidia klabu ile kufanya vizuri. Ningependa kuwa katibu wa ufundi, lakini sijui kama itakuwa pale Barcelona.

"Ningependa kurudi kwenye klabu na kuchangia chochote nitakachoweza, kwa sababu naipenda (Barcelona) na ningependa wao wafanye vizuri, kuendelea kukuwa na kuendelea kuwa moja ya klabu bora duniani."



# Klopp kuibomoa Leicester City

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ameripotiwa kuhusishwa na mpango wa kumsajili, Harvey Barnes kama mchezaji anayemuhitaji kwenye dirisha la uhamisho la msimu ujao wa majira ya joto kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye safu yake ya ushambuliaji.

Nyota huyu mwenye miaka 23, amekuwa sehemu muhimu sana ya kikosi cha Leicester kwa msimu huu wa 2021-22, akiwa amecheza jumla ya mechi 12 ambazo amefanikiwa kupata mabao mawili na kutoa asisti mbili.

Agosti mwaka huu, Barnes alisaini makubaliano mapya ya kusalia hapo kwenye dimba la King Power hadi mwaka 2025.

Taarifa zinaeleza kuwa klabu ya Liverpool itajaribu kumleta nyota huyo pale Anfield kuelekea msimu wa 2022-23.

Kwa mujibu wa ripoti, Klopp anamwona nyota huyo anafaa kuongeza jitihada kwa Sadio Mane, Roberto Firmino, Diogo Jota na Mohamed Salah kwenye safu ya ushambuliaji.



## HABARI MICHEZO


2,668,240

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Wolverhampton | 2.42 | 3.14 | 3.04 |
| 02. 06/11/21 | 18:00 | Blackburn vs Sheffield Utd | 2.32 | 3.29 | 2.89 |
| 03. 06/11/21 | 18:00 | Luton Town vs Stoke City | 2.27 | 3.21 | 3.06 |
| 04. 06/11/21 | 18:00 | Barnsley vs Hull City | 2.44 | 3.09 | 2.89 |
| 05. 06/11/21 | 20:30 | Alaves vs Levante | 2.55 | 3.05 | 2.95 |
| 06. 06/11/21 | 20:30 | Blackpool vs QPR | 2.44 | 3.28 | 2.74 |
| 07. 07/11/21 | 17:00 | Everton vs Tottenham | 2.65 | 3.15 | 2.75 |
| 08. 07/11/21 | 17:00 | Nantes vs Strasbourg | 2.38 | 3.23 | 2.98 |
| 09. 07/11/21 | 17:00 | Leeds vs Leicester | 2.85 | 3.45 | 2.39 |
| 10. 07/11/21 | 17:00 | Udinese vs Sassuolo | 2.47 | 3.44 | 2.75 |
| 11. 07/11/21 | 20:30 | Osasuna vs Real Sociedad | 2.94 | 3.24 | 2.43 |
| 12. 07/11/21 | 22:45 | Rennes vs Lyon | 2.89 | 3.48 | 2.32 |
| 13. 07/11/21 | 23:00 | Betis vs Sevilla FC | 2.80 | 3.21 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 02 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1062 | Wieczysta Krakow vs RKS Garbarnia Krakow | 1.82 | 3.56 | 3.71 |
| 15:00 | 2326 | MFK Dubnica vs Sport Podbrezova | 5.56 | 4.12 | 1.48 |
| 16:00 | 4874 | Kolubara vs Spartak Subotica | 2.59 | 3.12 | 2.54 |
| 16:00 | 5876 | Barnsley U23 vs Coventry U23 | 3.18 | 3.66 | 1.95 |
| 16:30 | 1410 | Kaizer Chiefs vs Stellenbosch | 2.24 | 3.00 | 3.34 |
| 16:30 | 5811 | Millwall U23 vs Watford U23 | 2.05 | 3.66 | 2.94 |
| 17:00 | 1662 | MC Alger vs CR Belouizdad | 2.65 | 2.94 | 2.61 |
| 17:00 | 1870 | JS Saoura vs RC Relizane | 1.43 | 3.81 | 7.33 |
| 17:00 | 5892 | Ol. Medea vs JS Kabylie | 2.13 | 2.88 | 3.51 |
| 17:30 | 5017 | Najma Manama vs Manama Club | 2.88 | 2.98 | 2.39 |
| 18:00 | 1592 | Metalac vs FK Napredak | 1.97 | 3.61 | 3.18 |
| 18:00 | 3425 | Widzew Lodz vs GKS Jastrzebie Zdroj | 1.39 | 4.24 | 6.94 |
| 18:00 | 5812 | Golden Arrows vs Moroka Swallows FC | 2.50 | 2.99 | 2.89 |
| 18:00 | 5951 | TS Galaxy FC vs Baroka FC | 2.44 | 2.85 | 3.14 |
| 18:30 | 2884 | Bloemfontein Celtic vs SuperSport Utd | 2.85 | 2.95 | 2.56 |
| 18:30 | 4837 | Orlando Pirates vs Sekhukhune United | 1.56 | 3.49 | 6.49 |
| 20:05 | 3168 | Riffa Club vs Al Ahli Manama | 1.34 | 4.43 | 7.89 |
| 20:45 | 1346 | VfL Wolfsburg vs RB Salzburg | 2.42 | 3.54 | 2.75 |
| 20:45 | 5570 | Malmo vs Chelsea | 14.02 | 7.01 | 1.18 |
| 21:00 | 1407 | Ponferradina vs Huesca | 2.72 | 2.91 | 2.72 |
| 21:00 | 3175 | Sporting Gijon vs Almeria | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 21:00 | 4350 | GIF Sundsvall vs Falkenbergs | 1.89 | 3.70 | 3.85 |
| 21:00 | 4975 | Landskrona Bois vs Osters IF | 2.55 | 3.30 | 2.75 |
| 21:15 | 1054 | Waterford Utd vs Derry City | 2.70 | 3.09 | 2.46 |
| 21:30 | 1535 | FC Stade LS Ouchy vs Yverdon-Sport FC | 1.61 | 4.03 | 4.32 |
| 22:45 | 1337 | Coventry vs Swansea | 2.08 | 3.39 | 3.29 |
| 22:45 | 1356 | Millwall vs Reading | 1.86 | 3.39 | 4.02 |
| 22:45 | 1542 | Charlton vs Rotherham | 3.33 | 3.38 | 2.07 |
| 22:45 | 1686 | Cliftonville Belfast vs Portadown FC | 1.31 | 5.80 | 8.20 |
| 22:45 | 1713 | Peterborough vs Huddersfield | 2.95 | 3.29 | 2.29 |
| 22:45 | 1831 | Luton Town vs Middlesbrough | 2.31 | 3.19 | 2.99 |
| 22:45 | 2212 | Fleetwood Town vs Wigan | 3.39 | 3.29 | 2.08 |
| 22:45 | 2499 | Morecambe vs Cambridge Utd | 2.41 | 3.33 | 2.74 |
| 22:45 | 2702 | Concord Rangers vs Dartford | 5.22 | 4.15 | 1.50 |
| 22:45 | 2970 | Birmingham vs Bristol City | 1.94 | 3.38 | 3.72 |
| 22:45 | 3075 | Portsmouth vs Cheltenham | 1.69 | 3.67 | 4.60 |
| 22:45 | 3127 | Woking vs Bromley | 2.54 | 3.57 | 2.43 |
| 22:45 | 3157 | Sheffield Wed vs Sunderland | 2.43 | 3.29 | 2.75 |
| 22:45 | 3747 | Larne vs Glentoran Belfast | 1.88 | 3.75 | 3.32 |
| 22:45 | 4070 | Nottingham vs Sheffield Utd | 2.75 | 3.24 | 2.45 |
| 22:45 | 5140 | Southend vs Dover | 1.82 | 3.67 | 3.81 |
| 22:45 | 5203 | Crewe vs Doncaster | 2.32 | 3.29 | 2.90 |
| 22:45 | 5248 | Wycombe vs Ipswich | 2.26 | 3.35 | 2.96 |
| 23:00 | 1892 | Villarreal vs BSC Young Boys | 1.54 | 4.41 | 5.41 |
| 23:00 | 3232 | Dynamo Kiev vs Barcelona | 4.59 | 3.82 | 1.72 |
| 23:00 | 3853 | Juventus vs Zenit St Petersburg | 1.61 | 3.89 | 5.51 |
| 23:00 | 3950 | Atalanta vs Manchester Utd | 2.59 | 3.66 | 2.50 |
| 23:00 | 4660 | Sevilla FC vs Lille | 1.65 | 3.74 | 5.39 |
| 23:00 | 4807 | Bayern Munchen vs Benfica | 1.18 | 7.57 | 12.95 |
| 23:15 | 4239 | Leganes vs FC Cartagena | 1.92 | 3.10 | 4.23 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# JUVE YAONGOZA KUMWANIA POGBA




**TURIN,** Italia

JUVENTUS imeripotiwa kuwa kinara katika mbio za mchakato wa kumsajili kiungo wa Manchester United, Paul Pogba mwishoni mwa msimu huu.

Mustakabali wa mwanasoka huyo wa Ufaransa kwa sasa bado haujawa wazi, kwani haijafahamika iwapo atasalia Old Trafford au ataamua kuondoka, huku klabu kama Real Madrid na Paris Saint-Germain zikionyesha nia ya kuipata huduma yake.

Hata hivyo, uwezekano wa kurejea Serie A kujiunga tena na miamba hao wa Italia, Juventus inaweza kuwa katika mipango ya nyota huyo kwa kuwa ndiyo klabu inayotajwa kuongoza mbio za kuinasa saini yake kwa mujibu wa Rudy Galetti.

Imeripotiwa kuwa Pogba hataongeza mkataba wake na Man United na ikiwa hivyo ndiyo atakavyofanya kurejea kwenye timu yake za zamani Italia ndio mpango alionao kwa sasa.

Kukamilisha mchakato huu, klabu hiyo inahitaji kumuuza mchezaji wa zamani wa Arsenal, Aaron Ramsey pamoja na Weston McKennie au Adrien Rabiot ili kumudu gharama ya mkataba wa euro milioni 12 kwa msimu pamoja na bonasi kwa mchezaji huyo wa 'Mashetani Wekundu'.



# *Vinicius kufungwa upya Real Madrid*

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wameripotiwa kuwa wapo tayari kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na Vinicius Junior kwa miezi ya hivi karibuni, baada ya miamba hao wa Hispania kuridhishwa na kiwango chake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amekuwa akionyesha kiwango bora pale kwa 'Los Blancos' msimu huu wa 2021-22, akifunga mabao tisa na asisti tano kwenye mechi 14 katika mashindano yote.

Vinicius bado amebakiza miaka minne kumaliza mkataba wake hapo Bernabeu, lakini ripoti ya majuzi ya gazeti la Marca zimedai kuwa Mbrazil huyo ni miongoni mwa wachezaji watano wanaolipwa mishahara midogo zaidi katika klabu hiyo licha ya umuhimu wake.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa habari za soka wa Italia, Fabrizio Romano akinukuliwa na Marca, Real Madrid wanajiandaa kufanya mazungumzo na mshambuliaji huyo kuhusu mkataba mpya.

Vinicius, ambaye anakadiriwa kukusanya kiasi cha euro milioni 4 kwa msimu kulingana na makataba wake wa sasa, alifunga mabao mawili dhidi ya Elche, Jumamosi, wakati vijana hao wa Carlo Ancelotti wakishinda 2-1 kwenye mchezo wa LaLiga.

Mchezaji huyo amefunga mabao 23 na asisti 28 kwenye mechi 132 akiwa Real Madrid tangu ahamie kutoka Flamengo, Julai mwaka 2018.

# Michezo



Jumanne Novemba 2, 2021
Nipashe

Redondo aitwa Stars kuivaa DR Congo UKURASA 20

UMEME!...



Mwamuzi Raphael Kambi kutoka Morogoro, akimuonyesha kadi nyekundu beki wa Simba, Henock Inonga Baka 'Varane', kwa madai ya kumpiga kichwa mchezaji wa Coastal Union, Abdul Hamisi, wakati timu hizo zikitoka suluhu kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Simba yawageukia mashabiki hofu sare

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

BAADA ya Simba juzi kubanwa mbavu kwa kulazimishwa sare ya pili mfululizo kwenye Ligi Kuu Bara kwa kutoka suluhu na Coastal Union ya Tanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, uongozi wa klabu hiyo na benchi la ufundi umewataka mashabiki wa timu hiyo kutulia kwani muda si mrefu kikosi chao kitakaa sawa na kuanza kufurahi.

Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Thierry Hitimana, aliliambia gazeti hili jana kuwa walicheza vizuri na kutengeneza nafasi, lakini walishindwa kuzitumia na kujikuta wanamaliza dakika 90 bila goli, hivyo wanaendelea kufanyia kazi mazoezini tatizo hilo na anaamini hali hiyo itaondoka mapema.

"Nafahamu matokeo haya hayakutegemewa, hata sisi benchi la ufundi hatupendezwi nayo, tunaendelea kufanyia kazi maungufu tuliyoyaona na naamini tutarejea kwenye mstari," alisema Hitimana.

"Bocco alipata nafasi, Denis (Kibu) alipata nafasi zaidi ya mbili, lakini nasema ndio mpira ulivyo, siku nyingine unacheza vizuri na unatengeneza nafasi lakini unakosa bahati," alisema.

Kauli hiyo pia iliungwa mkono Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, baada ya kuwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kutulia na kuendelea kuiunga mkono, kwani muda si mrefu hali itakuwa sawa, kwani hata msimu uliopita hawakuanza vizuri pia, lakini wakatwaa ubingwa. "Timu ilicheza vizuri kwenye mechi hii, lakini bahati haikuwa yetu. Nawasihi wanachama na mashabiki wa Simba kutulia," alisema Mangungu.

# YANGA, RUVU NI ZAIDI YA 'PIRA SAMBUSA' LEO

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### ●●● Miamba hiyo ya Pwani yapania kuwa ya kwanza kuitoboa, Nabi asema...

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, leo majira ya saa 12:15 jioni, kwa mara nyingine tena watashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kuikabili Ruvu Shooting, ambayo itakuwa ikijaribu kupata ushindi mara ya tatu mfululizo msimu huu.

Hata hivyo, Yanga inaingia uwanjani ikiwa si tu kwamba inaongoza ligi kwa kushinda mechi zake zote nne ambazo imecheza, lakini haijaruhusu bao lolote.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi, amesema kuwa timu yake inaingia uwanjani ikiwa imebadilika, huku akimsifu kocha wake wa mazoezi ya viungo, Helmy Gueldish kwa namna alivyowatengeneza wachezaji wake ambao awali walionekana hawana utimamu wa mwili pamoja na pumzi.

Alisema kuanzia mechi dhidi ya Azam wachezaji wa timu yake walionekana kubadilika, hivyo kwenye mechi ya leo dhidi ya Ruvu Shooting anatarajia kuona hali hiyo ikiendelea.

Pamoja na kwamba wanachama na mashabiki wa Yanga wanaona kikosi chao sasa kiko imara, Nabi alisema kuwa kuna makosa kidogo ambayo anayarekebisha ili timu iwe kwenye kiwango kikubwa zaidi ya ilivyo sasa.

"Bado kuna makosa nayarekebisha, yakikaa sawa, nina uhakika kabisa Yanga itakuwa tishio," alisema.

Lakini awali, makocha wasaidizi wa timu hizo, wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kwa upande wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wamejiandaa vizuri kuendelea walipoishia katika michezo iliyopita ya ligi hiyo.

Alisema licha ya kufanya vizuri katika michezo hiyo, lakini hawataingia uwanjani kwa kujiamini na washuka dimbani kwa tahadhari kubwa lengo likiwa ni kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Tumejiandaa vizuri licha ya kufanya vizuri na kupata matokeo, lakini kuna makosa yalifanyika na tumeyafanyia kazi, na sasa tuko tayari kuhakikisha tunaenda kutafuta pointi muhimu dhidi ya Ruvu Shooting," alisema Kaze.

Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Rajab Mohammed, yeye alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wako fiti tayari kwa mchezo huo. Alisema wanatambua Yanga ina wachezaji wazuri, lakini hawataingia kinyonge kwa sababu wamejiandaa vizuri kwenda kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo.

"Tumejipanga vizuri hatutaingia kinyonge kwa kuhofia Yanga, tuna waheshimu na tutakuwa wa kwanza kutikisa nyavu za wapinzani wetu hao na kurejea Mlandizi na pointi muhimu," alisema.

Naye Nahodha wa Ruvu Shooting, Ambros Renatus alisema mbinu, nguvu na kiufundi wako vizuri na tayari kuhakikisha wanapata alama muhimu katika mchezo huo.

"Tuko vizuri kwenda kutafuta, pointi katika mechi hii, sisi tutakuwa wa kwanza kwenda kuharibu furaha ya Yanga kwa kutikisa nyavu zao," alisema Ambros.

Mara ya mwisho timu hizo kukutana Yanga, ilitoka uwanjani kifua mbele baada ya kuichapa Ruvu Shooting mabao 2-1 kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mchezo mwingi wa ligi hiyo utakaopigwa leo ni kati ya Azam FC itakayoikaribisha Geita Gold FC katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >